# Nipashe

Ijumaa Novemba 13, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580398

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Wananchi wahudumiwe muda wowote, popote

Ukurasa 13

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 13, 2020 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 14

Ubunifu viwanda nchini sasa waibukia magari ya umeme

Milionea kijana aliyeacha wosia azikwe na gunia la fedha zake

Na Mwandishi Wetu

• Alitamba sana kwa 'pamba' nyeupe, sherehe
• Mchango wa mazishi yake umekuwa gumzo

MJUE Genius Kadungure, kijana wa umri miaka 36, yaani mzaliwa wa Oktoba 10, mwaka 1984, ikiwa ni miaka minne na nusu kamili tangu nchi yake kupata uhuru, amefariki dunia akiwa tajiri anayetikisa kitaifa na kimataifa.

Ndiye mfanyabiashara na Mwenyekiti anayemiliki kampuni ya Piko Trading Holdings, mwasisi wa Mfuko uitwao Genius Foundation, hali kadhalika anamiliki klabu ya maarufu ya usiku 'kujirusha' kwa jina Sankayi au maarufu Klabu ya Ndoto za |Maisha ya Usiku (Dreams Nightlife Club).

Darasani nako hajambo, kwani amekanyaga ardhi ya chuo kikuu mara kadhaa, akikwea hadi ngazi ya Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (MBA), kutoka Chuo Kikuu cha Great Zimbabwe, fani aliyoitendea haki katika maisha.

Katika jamii akijulikana zaidi kama Ginimbi, taarifa za msiba wake wa sasa, vyombo vya habari nchini humo sasa vinaripoti ya kuwapo wosia kwamba azikwe na gunia lililojaa fedha na gazeti la ...

UKURASA 11

**MZEE** afungwa jela miaka 30 kumbaka mtoto wa miaka 13

UKURASA 3



**MBATIA** ashauri maridhiano ili kudumisha amani

UKURASA 5

# Wabunge wapya wataja vipaumbele

## • Gwajima aahidi kuanza na mafuriko, mbunge wa CHADEMA alia upweke... *Endelea ukurasa 4*


Mbunge wa **Hai**, Saashisha Mafuwe


Mbunge wa **Nkasi Kaskazini**, Aida Khenani.


Mbunge wa **Muheza**, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA'


Mbunge wa **Buchosa**, Erick Shigongo


Mbunge wa **Kawe**, Josephat Gwajima


Mbunge wa **Vunjo,** Dk. Charles Kimei


Mbunge wa **Morogoro Kusini**, Hamisi Taletale 'Babu Tale'


Mbunge wa **Kinondoni**, Tarimba Abbas

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**LISSU ALONGA BAADA YA KUTUA UBELGIJI**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu...

UKURASA WA 5

**TAMWA YALAANI KUSHAMIRI UBAKAJI**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimelaani matukio ya ukatili wa...


## Spika aonya utoro bungeni

UKURASA 2



# Majaliwa: Sikutarajia kurudi uteuzi wa JPM

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **STARS KIBARUANI UGENINI TUNISIA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa, akitoa shukrani kwa Rais Dk. John Magufuli kwa kumpendekeza kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitishwa na wabunge kwa asilimia 100, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Majaliwa asema hakutarajia kurudi

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hakutegemea kama angerudi kwenye nafasi hiyo kutokana na kauli ya Rais John Magufuli ambaye mara kwa mara alikuwa akisema atashughulika na Baraza la Mawaziri.

Majaliwa aliyasema hayo jana katika mkutano wa kwanza wa Bunge la 12 jijini hapa baada ya kuthibitishwa na wabunge wote kwa kura ya siri kushika wadhifa huo kwa mara nyingine.

Jina la Majaliwa liliwasilishwa kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, na mpambe wa Rais likiwa kwenye bahasha iliyofungwa madhubuti.

Katika kura zilizopigwa jana za kumthibitisha Waziri Mkuu, Majaliwa alipata asilimia 100 ya kura zote za wabunge 350 waliokuwapo bungeni. Uchaguzi kama huo uliofanyika mwaka 2015, Majaliwa alipigiwa kura 258 sawa na asilimia 73.5, zilizoharibika zilikuwa mbili na za hapana zilikuwa 91.

Akizungumza baada ya kupigiwa kura, Majaliwa alisema tukio hilo limempa mshtuko na faraja kupita kiasi kwa sababu hakutarajia.

"Tulikuwa wote hapa, hakuna aliyekuwa na uhakika wa hili jambo. Lilipokuja limetushtua na niendelee kushukuru pamoja na utumishi wangu kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita mnakumbuka Rais John Magufuli kwa nyakati tofauti alikuwa akisema kwenye Baraza la Mawaziri lazima atashughulika nalo.

"Na mimi ni mmoja kwenye Baraza la Mawaziri, hakuna aliyekuwa na uhakika kwa hiyo hili jambo nimelipokea kwa mikono miwili. Ninamshukuru Rais na wabunge na chama changu," alisema huku akisisitiza kuwa kitendo cha kuthibitishwa kwake si jambo dogo na anaamini Mungu ndiye aliyeongoza.

"Ninamshukuru Rais Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kuwa imani kubwa juu yangu kuwa ninaweza kufanya yote ambayo tumeyafanya kwa miaka mitano na mingine mitano inayokuja," alisema.

Majaliwa alimshukuru pia Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kwa sababu anaamini kwa mamlaka ya Rais, atakuwa alimshirikisha kwenye kulipitisha jina lake kuwa Waziri Mkuu.

"Ninajua nitapata fursa ya kukutana naye (Rais Magufuli), nitamshukuru zaidi, Mungu amuongezee afya njema, uwezo na busara ili alitumikie taifa kwa weledi," alisema na kuahidi kumsaidia Rais Magufuli kadri Mungu atakavyomwongoza.

Majaliwa aliwaahidi wabunge kuwa bila kujali itikadi za vyama vyao, atapita katika majimbo yao kuona shughuli za maendeleo wanazozisimamia, kukagua miradi, kukutana na wananchi na kusikiliza kero zao ili zipate ufumbuzi.

Pia alisema atatoa ushirikiano kwa bunge kwa kupokea ushauri wa wabunge na kuyasikiliza yale yanayotoka kwenye majimbo yao.

"Niwaahidi wale wote watakaoteuliwa na Rais kushika nafasi ya Waziri na Naibu Waziri kwa niaba yao, tutawatumia wabunge wote ili malengo ya serikali tuliyojiwekea yawafikie wananchi," alisema.

**SPIKA WA BUNGE**

Baada ya kupigwa kura za kumpongeza, Spika Ndugai alisema: "Nakupongeza sana Waziri Mkuu kwa uteuzi huu. Tunamshukuru sana Rais kwa kuturudishia wewe. Tumefanya kazi pamoja miaka mitano tayari tunajuana, hivyo naamini tutakuwa na ushirikiano mkubwa zaidi huku tunakokwenda na hali ya utulivu bungeni itakuwa kubwa zaidi," alisema.

Alisema Bunge ndiyo sehemu ambayo siasa zinahamia kwa miaka mitano kutoka kwenye kampeni.

**MWANASHERIA MKUU**

Akiwasilisha hoja ya serikali kuhusu kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, alisema Majaliwa ni mzoefu katika nafasi hiyo na alitumikia kwa ufanisi mkubwa nafasi hiyo katika miaka mitano iliyopita.

Alisema Majaliwa ni mtu mwadilifu asiye na makuu na ana uwezo wa kubeba na kuhimili majukumu yote yanayoendana na wadhifa wake kwa mujibu wa Katiba.

"Ni mwenye hekima na busara nyingine, msikivu wa hali ya juu na mchapakazi hodari, anayemudu majukumu yake katika zama hizi za uwajibikaji, mwenye uwezo wa kuchambua kwa kina na kupima hoja mbalimbali zinapojitokeza," alisema.

Pia alisema Majaliwa ana umahiri katika kusimamia utendaji na kudhibiti nidhamu katika utumishi wa umma, mapambano dhidi ya rushwa na usimamizi bora wa sera za Taifa na uongozi bora wa serikali katika utekelezaji wa shughuli za bunge.

**JINA LILIVYOWASILISHWA**

Mpambe wa Rais, Kanali Benard Mlunga, alifika Bungeni saa 09.53 asubuhi akiwa na begi dogo la mkononi.

Baada ya kuingia bungeni, mpambe huyo alimwambia Spika huyo kuwa ameagizwa na Rais kuwasilisha kwake nyaraka hiyo yenye jina la Waziri Mkuu.

Mpambe huyo alifungua begi hilo na kutoa bahasha nyeupe na kumkabidhi Spika Ndugai ambaye alisema imegongwa mihuri sita ya siri.

Spika Ndugai alimkabidhi Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, kufungua bahasha hiyo mpambe huyo akiwa pembeni na baada ya kufungua alimkabidhi bahasha hiyo Spika na kutoa nyaraka mbili zenye jina la Waziri Mkuu.

Baada ya kutoa Spika aliwaonyesha wabunge huku akisema kuna barua mbili na kuzitia saini kuthibitisha kupokea na kumkabidhi nakala moja ili kumrejeshea Rais ikiwa na jina la Waziri Mkuu mteule.

Saa 09.57 asubuhi, mpambe huyo aliondoka katika eneo la Bunge kwa ajili ya kurudi kwa Rais kurudisha majibu kuwa ujumbe aliyopewa umefika na umepokelewa na wahusika.

Baada ya hapo Spika Ndugai alikohoa kidogo kabla ya kutaja jina hilo na baadaye alisoma kilichoandikwa ndani.

Spika Ndugai alisema kuwa kwa mujibu wa Katiba Rais baada ya kuchukua madaraka yake ndani ya siku 14 atachagua mbunge anayetokana na chama chenye wabunge wengi bungeni na anayeungwa mkono kuwa Waziri Mkuu.

Baada ya maelezo hayo alimtaja Kassim Majaliwa kuwa ndiye aliyeteuliwa na Dk.John Magufuli kuwa Waziri Mkuu ambapo wabunge walilipuka na shangwe na vifijo huku wengine wakienda kumpongeza baada ya kusikia jina.

**■Imeandaliwa na Romana Mallya na Agusta Njoji (DODOMA)**

# Spika aonya utoro bungeni

**Na Waandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewaonya wabunge watoro bungeni na kuhadharisha kuwapo na mitambo ya kutambua mahudhurio yao.

Pia, ameonyeshwa kusikitishwa na vyama vya upinzani ambavyo vimegoma wabunge wao kuhudhuria bungeni ikiwamo wa viti maalum kwamba vinawanyima fursa ya kuwatetea Watanzania. Ndugai aliyasema hayo jana bungeni muda mfupi baada ya wabunge kupiga kura ya kumchagua Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson.

Alisema suala la mahudhurio ni muhimu na kuna mitambo ya kila aina ya kujua mahudhurio yao na taarifa zinatunzwa.

"Kwa kuwa safari hii chama kikubwa ndicho chenye wabunge waliowengi ni rahisi kudhibiti nidhamu ya hilo, ni rahisi kupeleka kwenye chama kuwa hawa ndiyo watoro, kwa hiyo tujitahidi sana kama una udhuru tunajua, mbunge una mambo mengi sana, tunakuomba uhudhurie," alisema.

**VITI MAALUM**

Spika Ndugai alisema kuna vyama vimegoma kupeleka wabunge wao bungeni licha ya kuwa na fursa hiyo hasa wa viti maalum.

"Kuna makundi matatu ambayo bado wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, tutawapata kwenye mkutano ujao, kuna wabunge 10 wa kuteuliwa na rais ambao tutawapata tu kadri atakavyoteua, pia kuna viti maalum kupitia vyama vya siasa. "Vipo vyama ambavyo bado havijaleta wabunge wao, tunachokiona kwenye mitandao na mahali pengine, wanalumbana kutowaleta wabunge. Zingekuwa nafasi za wanaume wangewaleta siku nyingi hapa, wapigakura nchi nzima ndiyo muelewe hivi vyama ni shida."

Alisema suala hilo halikubaliki na halipaswi kuwa mjadala. "Wanatakiwa kubadilika kidogo siyo vitu vya kubishania kwa kuwa ni fursa, akidi ipo mkiitumia hiyo nafasi ni vyema, wasipoitumia kama kawaida bunge litaendelea," alisema.

**KAMATI ZA BUNGE**

Kuhusu kuundwa kwa Kamati za Bunge, Spika aliwasisitiza wabunge kujaza fomu za maelezo binafsi ili kusaidia upangaji wa kamati.

Alibainisha kuwa kamati hizo zitaundwa katika bunge lijalo baada ya rais kuunda serikali na zitaendana na sekta kwa namna serikali ilivyounda.

"Kutakuwa na uchaguzi unaoendelea ikiwamo uwakilishi katika Bunge la SADC (Jumuiya ya Maendeleo kwa Nchi za Kusini mwa Afrika), EAC (Jumuiya ya Afrika Mashariki) na Maziwa Makuu, msijione wanyonge kugombea kwa sababu ni wageni, hapana kila bunge linajitegemea ni la 12, sisi sote ni sehemu moja," alisema.

Alisema kutakuwa na uchaguzi wa wenyeviti na makamu wa wenyeviti wa kamati huku akishauri kwenye halmashauri wabadili utaratibu, ili kuhakikisha mwanamke anashiriki kwenye nafasi moja wapo kati ya Meya au Naibu Meya.

**TULIA AULA TENA**

Akitangaza kura alizopata Dk. Tulia, Spika Ndugai alisema amechaguliwa kwa kura 350 kati ya 354 kuwa Naibu Spika wa Bunge.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Dk. Tulia aliwashukuru huku akiahidi kufanya kazi kwa uaminifu kumsaidia Spika ili kuishauri na kuisimamia serikali. Aliahidi pia kushirikiana na wabunge na kuwashauri pale watakapohitaji kushauriwa.

**JPM KUHUTUBIA BUNGE**

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, alisema kutokana na Rais John Magufuli kuhutubia na kuzindua Bunge la 12, ametengua kanuni ili kuruhusu viongozi hao maalum walioruhusiwa na Spika kuingia kwenye ukumbi.

**■Imeandaliwa na Augusta Njoji na Romana Mallya (DODOMA).**

## HABARI KITAIFA

# Mzee miaka 50 jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita, imemhukumu mkazi wa Nyakumbu Juma Kisinza (50), kifungo cha miaka 30 jela pamoja na viboko 12 kwa kosa la kumbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 13.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya upande mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na wazee wengine wenye tabia kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clemence Kato, ulipeleka mahakamani mashahidi wanne pamoja na kielelezo kimoja ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Alisema siku ya tukio hilo Julai 9, mwaka huu, majira ya usiku mwanafunzi huyo akiwa amelala chumbani na wadogo zake, mshtakiwa aliingia kupitia dirishani na kumwambia mwanafunzi huyo kuwa anataka ampe dawa ya kupaka sehemu zake siri, msichana huyo alikataa ndipo mshtakiwa huyo alipomshika kwa nguvu na kuanza kumbaka huku akimtishia kuwa akipiga kelele atamuua.

Alisema wakati akimfanyia kitendo hicho cha kinyama, mwanafunzi huyo alipiga kelele na mama yake mzazi aliende chumbani na kumkuta mshtakiwa akimbaka mwanawe.

Alisema mama mzazi alichukua mpini na kumpiga mshtakiwa huyo mgongoni huku akipiga kelele za kuomba msaada kwa majirani ambao walifika na kumkamata mshtakiwa huyo na kumpeleka katika kituo cha polisi.

Hakimu huyo alisema mwanafunzi huyo alipelekwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Geita na alipofanyiwa uchunguzi alikutwa na michubuko pamoja na manii sehemu za siri za mwanafunzi huyo.

Hakimu Maweda alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote, na kumtia hatiani mshtakiwa kwa kosa hilo.

Mshtakiwa huyo aliangua kilio na kudai kuwa yeye ana watoto wana mtegemea hivyo anaomba mahakama hiyo impunguzie adhabu.

Akitupilia mbali utetezi huo, Hakimu Maweda alisema mshtakiwa akiwa na umri wa miaka 50 kuingia chumbani kwa kupitia dirishani na kumbaka msichana mwenye umri wa miaka 13 ni kitendo cha kinyama kwa mtu mzima mwenye akili timamu.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Clemence Kato, alidai, Julai 9, mwaka huu, mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo.

# Lissu alonga baada ya kutua Ubelgiji

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema hajaomba ukimbizi nchi yoyote, bali amerudi Ubeligiji kwa kuwa aliishi huko kwa miaka mitatu.

Lissu, aliyewania urais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliopita na kushika nafasi ya pili nyuma ya mshindi, Dk. John Magufuli, pia ametamba kuwa hajakimbia mapambano bali amebadili mbinu na eneo la kufanyia mapambano yake.

Alitoa kauli hiyo alipohojiwa na DW na BBC kwa nyakati tofauti baada ya kutua Ubelgiji, akidai kuwa majadilino ya serikali na baadhi ya mabalozi ndiyo yamemwezesha kuondoka nchini.

"Kukimbilia nje ni mbinu ya zama zote za wanaopigania haki au kudai haki, ikifika mahali wanakimbilia huko," Lissu alisema.

Alisema vitisho dhidi yake havikuwa vya kupuuza kwa kuwa miaka mitatu iliyopita alivipuuzia na kuishia kupigwa risasi.

Alisema ameondoka nchini kama raia huru wa Tanzania na anakwenda Ubeligiji kama mkazi mwenye kibali cha kuishi.

"Ninakwenda Ulaya kwa ajili ya kujipanga upya na kuzungumza na jumuiya za kimataifa juu ya masuala ya Tanzania kuanzia sasa kwenda mbele, Uchaguzi Mkuu na yaliyotokea na maana yake kwa siku zijazo," alisema.

"Mapambanao bado yanaendelea, ni uwanja wa mapambano unabadilika kidogo, mimi ni kiongozi wa chama, nitahudhuria vikao vyote vinavyonihusu kwa njia ya mtandao, nitaendelea kujihusisha na masuala ya Tanzania, sikimbii nchi, sikimbii mapambano bali tunabadilisha uwanja na mbinu za mapambano," alisema.

Lissu alisema hatakuwa mtu wa kwanza kwenda kufanya harakati nje ya nchi na kwamba wapo viongozi wengi wamekuwa wakimbizi wa kisiasa na walirudi nchini mwao.

Msemaji wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alipoulizwa na BBC kuhusu suala hilo, alisema uchaguzi umekwisha na kwa sasa watu wanafanya maendeleo na kwamba wapinzani wanafanya maigizo.

"Madai ya wapinzani siyo mapya, yamekuwa ni maigizo yao kila mwaka, wanaposhindwa kwenye medani za kidemokrasia wanatunga uongo, uzushi. Kwa hiyo, hili jambo siyo jipya ndiyo maana unaona Watanzania wamepuuza, wanaendelea na shughuli zao.

"Haiwezekani ukajiamualia umeamka asubuhi unataka kuwa mkimbizi, ninachotaka anayesema ametishiwa, aseme ametishiwa na nani, lini na wapi? Hao anaosema wametishiwa, wametoka kufanya uchaguzi, wamefanya kampeni kwa siku 60, wamelindwa na kuwa salama," alisema.

Wiki iliyopita, aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, alikamatwa eneo la Kajiado nchini Kenya alikokimbilia kutafuta hifadhi yeye na familia yake na baadaye aliachiwa kwa ajili ya kuendelea na safari yake ya kutafuta hifadhi ya kisiasa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga (Same – Mwanga WSSA) ("Muombaji") kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Same na Mwanga, pamoja na sehemu za Halmashauri za Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe zilizopitiwa na mradi wa maji safi Same - Mwanga – Korogwe. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji yametolewa kama ifuatavyo:-

| |
|---|
| **1: Jina na Anuani:** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga (Same - Mwanga WSSA),<br>S.L.P 71,<br>Mwanga.<br>Tanzania.<br>Barua Pepe: mdsamemwanga@maji.go.tz |
| **2: Maelezo ya Leseni:** |
| Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Same na Mwanga, pamoja na sehemu za Halmashauri za Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe zilizopitiwa na mradi wa maji safi wa Same - Mwanga – Korogwe |
| **3: Vyanzo vya Maji na Miundombinu** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga ina vyanzo vikuu vya maji vya aina mbili ambavyo ni maji ya visima na maji ya chemchemi. Same - Mwanga ina jumla ya visima saba (7) ambavyo vina uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 5,450 kwa siku na vyanzo vingine viwili (2) vya chemchemi vyenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 111 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji inajumuisha; matenki ya maji kumi na nne (14) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 1,609. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 139.92, pamoja na vilula 65. |
| **4: Umiliki** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

# Wabunge wapya wataja vipaumbele

## ■Gwajima kuanza na mafuriko ya Dar, Mbunge CHADEMA alia upweke...

**Na Waandishi Wetu**

WABUNGE wapya wamebainisha vipaumbele watakavyoanza navyo katika kuwatumikia wananchi, huku Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima (CCM), akitamba kuanza kushughulika na kero ya mafuriko jijini Dar es Salaam.

Wakizungumza na Nipashe kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma kwa nyakati tofauti, wabunge hao walitaja mambo mbalimbali ambayo wamejipanga kuyasimamia wakiwa kwenye chombo hicho.

**ASKOFU GWAJIMA**

Mbunge huyo wa Kawe alisema jambo la kwanza analoanza nalo kwa wananchi wake ni kutatua kero ya mafuriko ambayo imedumu kwa muda mrefu maeneo mbalimbali jimboni huko.

"Tutashughulika na mafurikio ambayo mvua zinaponyesha zinasababisha wananchi wangu kukosa pa kukaa, tutashughulika na miundombinu ya ndani na tatizo la maji," alisema.

**ABBAS TARIMBA**

Mbunge huyo wa Kinondoni (CCM), alisema walifanya tathmini na kubaini kwamba kuna mambo atapaswa kuyafanya licha ya kuwa nje ya ilani ya chama chao.

"Tutatengeneza mipango ya sasa, ya kati na ya muda mrefu na tutaitekeleza kwa kuangalia wapi tumetoka, tulipo na tunakoelekea ili kuzitatua kero za wananchi," alisema.

**KHAMIS MWINJUMA 'MWANAFA'**

Mbunge huyo wa Muheza (CCM), alisema wasanii wenzake wasiwe na wasiwasi naye kwa kuwa atahakikisha hawaangushi katika kutatua kero za Muheza kuharakisha maendeleo.

**HAMISI TALETALE 'BABU TALE'**

Mbunge huyo wa Morogoro Kusini (CCM), aliwahakikishia Watanzania kuwa anakwenda kujenga hoja bungeni na siyo kupinga kila kitu.

"Haimaanishi tukiwa wabunge wengi wa chama kimoja, basi tutakuwa wabunge wa ndiyooo... Bunge litakuwa ni lenye kujenga hoja, binadamu yeyote kama ameumbwa kupinga, atapinga tu," alisema.

**AIDA KHENAN**

Wakati wabunge hao wa chama tawala wakitamba kufanya hayo, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema anaamini atakuwa mpweke katika Bunge hilo kwa sababu alitamani kujifunza mengi zaidi kupitia wabunge wa chama chake, ili kuongeza uzoefu, lakini hawapo tena bungeni.

"Ila kama wabunge wote tumekuja bungeni kuwakilisha wananchi, ninaamini tutaunganishwa na fikra zetu ambazo ni za wananchi wetu, tunajua walio wengi wataamua," alisema.



Kijana akiruka kuvuka upande mmoja kwenda mwingine baada ya daraja lililokuwa eneo la Tabata Kisukuru maarufu kama kwa Banyenza kusombwa na maji kufuatia mvua kubwa iliyonyesha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

Kuhusu kipaumbele chake jimboni, Khenan alisema ni kujenga njia shirikishi ili kuleta maendeleo kwa kutumia wadau.

"Kipaumbele changu cha kwanza ni maji ambayo bado ni tatizo, tunategemea kutumia njia tofauti kuhakikisha huduma hii inapatikana jimboni kwa kutumia njia ya uhakika, hili tayari nilishalishauri awali, nitaliendeleza," alisema.

Mbunge huyo alisema kipaumbele cha pili ni kilimo, akiahidi kushughulikia kero katika upatikanaji wa pembejeo ambayo ni kubwa kwenye sekta hiyo.

"Ninategemea kuunda timu ya wadau wa maendeleo jimboni kwangu ili kushughulikia masoko ya ndani na ya nje," alisema.

**GODFREY MWAMBE**

Aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji (TIC) ambaye sasa ni Mbunge wa Masasi Mjini (CCM), Godfrey Mwambe, aliwaahidi wapigakura wake kuwa hatawaangusha.

"Sitawaangusha kwa sababu mwongozo tumepewa wa kichama kwamba ni lazima tuisaidie serikali na siyo kukaa kimya au kutotoa hoja, pia kuboresha hoja za serikali na kuhakikisha zinaakisi matakwa ya wananchi," alisema.

Mbunge huyo alisema ni lazima kuisaidia serikali kwa kwenda bungeni na hoja zenye kujenga na kuboresha mipango ya serikali.

"Tunatakiwa tuseme na wananchi wayasemee, mbunge kazi yake kubwa ni uwakilishi," alisema na kufafanua kuwa mikoa ya kusini inalima korosho na kwamba kinachotakiwa kuboreshwa kwenye sekta hiyo ni upatikanaji wa pembejeo.

"Pembejeo zinachelewa, bei ni kubwa lakini kuna walanguzi wengine, pembejeo nyingine zinaua korosho, lakini mfumo wa soko bado siyo mzuri, lazima tujenge msingi imara wa kubangua korosho zote na kutengeneza bidhaa ndogo zinazotokana na korosho, ili kutengeneza thamani kubwa," alisema.

**ERICK SHIGONGO**

Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo, alisema wananchi wa jimbo hilo wamepata mbunge anayejua shida zao ikiwamo barabara na fursa za kibiashara.

**HAMIS TABASAMU**

Mbunge huyo wa Sengerema (CCM), alisema wananchi watarajie kufanyiwa makubwa ikiwamo kuondoa tatizo la mrundikano wa wanafunzi darasani na uhaba wa walimu shuleni.

**DOROTHY KILAVE**

Mbunge huyo wa Temeke (CCM), alisema yale yote aliyoahidi na yaliyoko kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM yatatekelezwa jimboni kwake.

**SALIM HASHAM**

Mbunge huyo wa Ulanga (CCM), aliahidi kutimiza aliyoahidi ikiwamo kupeleka zana za kilimo cha kisasa jimboni ili vijana wajishughulishe na kilimo.

Alisema wabunge wakitambua wajibu wao, italeta chachu kwa serikali kuleta maendeleo yenye tija.

**JESCA MSAMBATAVANGU**

Mbunge huyo wa Iringa Mjini aliyemshinda Mchungaji Peter Msigwa, alisema amejipanga na ana mikakati mizuri kwa ajili ya wananchi wake.

Alitaja mipango hiyo kuwa ni pamoja na kuwekeza katika elimu ya ujasiriamali ili kujiletea maendeleo kwa mtu mmoja mmoja.

"Wananchi wa Iringa wamepata mwakilishi bora, atawasilisha kero kwa serikali na zitatatuliwa kwa wakati," alitamba.

**STEPHEN BYABATO**

Mbunge huyo wa Bukoba Mjini (CCM), alisema atakuwa mwakilishi mzuri wa wananchi na anaamini Bunge hilo litakuwa chachu ya maendeleo kwa kuwa wabunge waliopo watakuwa wajenzi wa hoja zenye tija.

"Lengo ni kufanikisha maendeleo ya wananchi, nina uwezo wa kusema, kujenga hoja na kuwatetea wananchi ili kupata mahitaji ambayo tulitangaza wakati wa kuomba kura," alisema.

Alisema vijana wapo wengi bungeni na wameaminiwa na wananchi huku akitaja sifa ya kushinda vijana ni kutokana na wapigakura wengi kwa sasa kuwa ni kundi hilo.

**GODWIN KUNAMBI**

Mbunge huyo wa Mlimba (CCM) alisema kipaumbele chake cha kwanza ni kuhakikisha ndani ya miaka mitano Mlimba inakuwa na barabara ya lami. "Ninakwenda kujenga hoja zenye tija kwa taifa, watu wa Mlimba kuhakikisha mikoa ya Njombe, Ruvuma inaunganishwa na Morogoro kwa kiwango cha lami," alisema.

**SAASHISHA MAFUWE**

Mbunge huyo wa Hai (CCM), alisema kazi imeanza baada ya uchaguzi kumalizika na kwamba wananchi wa jimbo hilo wamemtuma mambo mengi ya kuwasemea bungeni.

"Zipo kero za kutosha kwenye suala la maji, barabara, ni imani yangu tunaenda kuzitatua zote kwa kuwa ziko kwenye ilani ya uchaguzi, kazi yangu ni kuunganisha serikali na wananchi tuende kwa kasi, yale niliyokuwa ninazungumza, naenda kuyafanya kwa vitendo," alisema.

Alisema kipaumbele cha jimbo hilo ni kilimo na viwanda, hivyo dhamira yake ni kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja kupitia kilimo na viwanda.

"Kama mnavyojua Jimbo la Hai tumekuwa kwenye upinzani takribani miaka 20, kwa hiyo wana kiu kubwa ya kuona utekelezaji wa ilani ya uchaguzi nitasimamia utekelezaji kwa asilimia 100, lakini kuisimamia serikali kutekeleza ahadi zilizotolewa na viongozi wakuu kwenye kampeni, kwa kasi kubwa tunaenda kuonyesha tofauti ya kuchagua CCM," alisema.

Alisema kwa sasa anapita kata zote kuwauliza wananchi mambo ambayo wanataka wawakilishiwe bungeni.

"Ninachofanya kwa sasa kabla ya kuapishwa, nimeanza kuzunguka baadhi ya kata na kuzungumza na wananchi ili ni mambo gani wanataka niwawakilishie bungeni," alisema.

Mafuwe pia alimkaribisha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Freeman Mbowe, kumpa ushauri na maoni yake kwa kuzingatia Ilani ya CCM.

"Yule ni mwananchi katika jimbo langu na anazo heshima kama kiongozi mstaafu wa Jimbo la Hai," alisema.

**DK. CHARLES KIMEI**

Mbunge huyo wa Vunjo, alisema jimbo hilo limekaa chini ya upinzani kwa zaidi ya miaka 10 na wako nyuma kimiundombinu ya kiuchumi na huduma za jamii.

Alisema uchaguzi huu wakazi wa Vunjo wamepiga bingo kwa kuwa wamechagua mtu sahihi.

"Ninawashukuru wananchi wamekuwa wajasiri kuendelea kukaa chini kwa watu ambao hawatekelezi, miundombinu imerudi nyuma kwa kuwa haikukarabatiwa, wapinzani hawakuwa wanajituma kushughulikia kero za wananchi," alisema.

Dk. Kimei alisema atashughulikia tatizo la ajira kwa vijana kwenye jimbo hilo ambao wamekuwa wakikaa kwenye vijiwe na kujifunza mambo ya uhalifu.

"Ajira haitokani na serikali tu bali ajira kubwa itatokana na sisi wenyewe kujiwezesha na kuonyeshwa fursa zinazofanyika kwenye ulimwengu wa viwanda, sisi ambao tumetumikia nchi na kujenga taasisi kubwa, tunajua fursa zipo wapi na miradi gani midogo ifanyike ambayo itazalisha ajira," alisema.

Dk. Kimei alisema mashine ndogo ya kutengeneza tomato inatoa ajira kwa watu watatu, hivyo ni sehemu ya mifano lukuki katika mipango yake ya kuzalisha ajira kwa wananchi.

"Nimeahidi nitatumia muda mwingi kuzungumza nao kufanya vitu vya moja kwa moja vitakavyowasaidia ili kupata fedha na ajira, nitakachofikisha cha kwanza ni kutengeneza ajira," alisema.

# Mbatia ashauri maridhiano baada ya uchaguzi

**Na Edwin Mhagama**

MWENYEKITI wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, ameshauri yafanyike mazungumzo ya maridhiano ya kitaifa yatakayohusisha viongozi wote wa kitaifa bila kujali itikadi ya kisiasa, dini au kabila.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari alipokuwa anatoa tathmini ya chama chake kuhusu Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Mbatia alisema taifa linapaswa kukubaliana kuwa kitu kimoja kwa maslahi ya nchi na kwamba wenye dhamana ya kufanyika kwa maridhiano hayo ni viongozi waliopo madarakani.

"Sisi NCCR Mageuzi tunahimiza meza ya mazungumzo ya kupata muafaka wa kitaifa wa kututoa hapa tulipo, rai yetu kuanzia sasa viongozi wote kijamii, kisiasa, kidini au taasisi yoyote tutumie ndimi zetu kwa kuifanya Tanzania kuwa sehemu salama na nzuri zaidi ya kuishi," alisema Mbatia

Mbatia aliongeza kuwa maridhiano yanapaswa kutoa kipaumbele kwa wananchi na taifa la Tanzania kwa ujumla.

"Tukubali kwamba maslahi ya Tanzania kwanza na mengine badaye na siyo kwa madaraka yetu ya kisiasa au ubinafsi wa mtu yeyote Yule," alisema Mbatia

Mbatia alisema kumekuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu nchini hasa wakati au baada ya uchaguzi mkuu, akitoa mfano wa haki msingi ya kupata taarifa huku akitolea mfano kwa tatizo la kukosekana kwa mtandao wa intaneti mara baada ya uchaguzi.

Awali, kabla ya kutoa tathimini ya uchaguzi uliopita, Mbatia alitoa pole kwa viongozi na wanachama wa Chama cha ACT Wazalendo kutokana na kifo cha aliyekuwa mwakilishi mteule wa Jimbo la Pandani Pemba, Abubakar Khamis Bakar kilichotokea usiku wa kuamkia Novemba 11, 2020.




Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Godwill Wanga, akizungumza kwenye uzinduzi wa mkutano wa masuala ya uongozi ujulikanao kama 'Leadership Summit 2020', ulioandaliwa na Taasisi ya Kingdom Leadership Network Tanzania (KLNT), kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Regent cha Marekani, ambao utatoa kozi ya wiki 14, kuhusu mafunzo ya biashara, uongozi na ujasiriamali ili kujua maadili ya uongozi kwenye biashara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yalaani kushamiri ubakaji

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimelaani, matukio ya ukatili wa kijinsia yanayoendelea nchini, ikiwamo tukio la mwanafunzi wa darasa la sita, kupewa ujauzito na mwenyekiti wa kijiji.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, aliyasema hayo jana kwenye taarifa yake kuwa matukio kadhaa ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa hivi karibuni na vyombo vya habari ikiwamo ubakaji, yanaashiria vitendo hivyo vinaendelea, licha ya sheria, matamko na sera kupinga matukio hayo.

Alisema miongoni mwa matukio hayo, ni la Novemba 11, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ijinga, Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, Badri Masengo (40), anayedaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la sita, mwenye umri wa miaka 15.

"Tukio lingine ni lile la mtoto wa miaka sita, jijini Arusha, aliyebakwa hadi kufa, Julai mwaka huu. Wakati huo huo, mtoto wa miaka 12 wilayani Serengeti, alibakwa na kujeruhiwa vibaya, Januari 12, mwaka huu," alisema Rose.

Pia alisema, tukio lingine la juzi ni kubakwa kwa mwanafunzi wa mwenye umri wa miaka 10 na mwalimu wake, Anderson Eneza (27).

Akielezea matukio mengine, Rose alisema ni Medadi Chitezi (60) mkazi wa kijiji cha Ulumi, mkoani Rukwa, kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto wa miaka 10, kosa alilolifanya Agosti, 12, mwaka huu.

Pia kwa upande wa Zanzibar, alisema liliripotiwa tukio la Haroub Abdallah Hamad (60), akidaiwa kumbaka mtoto wa miaka mitano, tukio lililotokea Oktoba 10, mwaka huu, wilayani Wete, Pemba.

Rose alisema matukio hayo na ambayo bado hayajaripotiwa ni dhahiri kuwa bado vitendo hivyo vinaendelea nchini, pamoja na sheria zinazopinga na kutoa adhabu kwa watuhumiwa.

"TAMWA ambayo miongoni mwa malengo yake makuu ni kuzuia na kupunguza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, inalaani vikali kuendelea kwa matukio hayo katika jamii.

Watoto wana haki ya kulindwa na kuishi kwa furaha, kama binadamu wengine na kibaya zaidi ni kuwa watoto wanabakwa wengine wanapoteza maisha kutokana na kufanyiwa ukatili, kujeruhiwa na kuathirika kisaikolojia hata kuharibiwa mustakabali wa maisha yao," alisema Rose.

Kadhalika, alisema ripoti ya Taasisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) ya mwaka 2017, ilieleza katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2016, kuripotiwa kesi 10,551 za uhalifu dhidi ya watoto, kati yake za ubakaji zikiwa 4,423.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18. Sheria hii ya mtoto inakataza ubaguzi na ukatili wa aina yoyote dhidi ya watoto. TAMWA tunaiomba serikali kuendelea na vita hii dhidi ya ubakaji hasa wa watoto, kwani hiki ni kizazi kijacho chenye manufaa tarajiwa katika ujenzi wa nchi yetu," alisema Rose.

Alisema, TAMWA inaipongeza serikali na mahakama kwa kusimamia kesi za ubakaji kwa umahiri, ikiwamo za ubakaji wa watoto ambazo zimefanyiwa kazi kwa kipindi kifupi na kutolewa hukumu pamoja na ambazo zimefikishwa mahakamani na kufanyiwa kazi na maofisa usalama.

"TAMWA tunasisitiza uwazi na uwajibikaji katika kuripoti masuala ya ubakaji wa watoto. Kila mmoja atimize wajibu wake, familia, jamii na watoto wenyewe wafundishwe kuvunja ukimya.

Wadau watumie nafasi walizonazo katika kuhakikisha ubakaji huu unamalizwa. Serikali itimize wajibu wake kisheria katika usimamizi wa kesi za ubakaji kwa wakati," alisema Rose.

# Mwanafunzi afa, watatu wajeruhiwa

**Na Steven William** MUHEZA

WANAFUNZI wanne wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Cheif Mang'enya wamegongwa na gari dogo na kusababisha mmojawao kufariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa.

Tukio hilo lilitokea jana majira saa 2:00 asubuhi katika eneo la shule hiyo wilayani hapa wakati wanafunzi hao wakitoka nyumbani kwenda shuleni.

Wanafunzi hao walikuwa wameongozana wakitembea kwa miguu katika barabara kuu ya Tanga kuelekea Muheza mpaka Segera. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, alisema wanafunzi hao waligongwa na gari dogo aina ya Toyota Mark X lenye namba za usajili T 906 DEP lililokuwa likiendeshwa na dereva aliyefahamika kwa jina moja la Mwangosi akiwa anakwenda Tanga mjini.

Chatanda alimtaja mwanafunzi aliyefariki dunia kuwa ni Mariam Mubaraka (16) anayesoma kidato cha tatu na mwili wake umehifadhiwa katika chumba cha maiti Hospitali ya Teule ya Wilaya ya Muheza kusubiri taratibu za mazishi. Alisema katika ajali hiyo, wanafunzi watatu wamejeruhiwa vibaya sehemu mbalimbali za miili yao na wamelazwa kwenye wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) ya hospitali hiyo.

Kamanda Chatanda aliwataja wanafunzi hao kuwa ni Elia Binde anayesoma kidato cha kwanza, Elisha Binde (kidato cha tatu) na Mwanahamisi Mariki pia wa kidato cha tatu. Shuhuda wa ajali hiyo, mkulima wa shamba eneo la karibu na shule, Elias Tendwa, mkazi wa kijiji cha Genge, alisema wanafunzi hao walifika karibu na shule wakiwa wamechelewa namba shuleni ndipo walichungulia na kuwaona walimu wapo wanawasubiri.

Alisema kuwa wanafunzi hao walitumia mbinu yao ya kila siku wanapochelewa namba waliamua kurudi nyuma watumie njia ya kujificha ili waingie darasani bila walimu wao kuwaona ndipo waliporudi katika barabara ya lami ili watumie njia nyingine kupitia katika kipori cha majani waingie darasani.

Wakati wanatembea katika barabara hiyo kuu, ghafla waligongwa na gari dogo kwa nyuma yao na hatimaye mmoja kupoteza maisha.

Tendwa alisema kuwa dereva wa gari hilo aligeuza na kurudi katika kituo cha polisi Muheza kutoa taarifa kwamba amepata ajali.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Chief Mang'enya, Ramadhani Kabelwa, alithibitisha wanafunzi wake kugongwa na mmoja kupoteza maisha na kuongeza kuwa waliojeruhiwa wako mahututi na wamepelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Bombo mjini Tanga kwa matibabu zaidi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ubakaji tishio kwa jamii, lazima tuchukue hatua

**MATUKIO** ya ubakaji, ulawiti na ukatili dhidi ya watoto yanaongezeka kila siku, na yanaibuka mapya ambayo yametendeka katika jamii jambo linalodhihirisha kuna kazi kubwa ya kufanya ili kulinda haki za watoto. 'Mathalani, katika gazeti la leo tumechapisha habari ya hukumu dhidi ya baba wa miaka 50 aliyehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na viboko 12 kwa kosa la kumbaka mwanafunzi wa miaka 13.

Baba huyo aliingia ndani ya nyumba hiyo kupitia dirishani na kumdanganya msichana huyo kuwa anadawa ya kuweka sehemu za siri na kumuingilia na kumsababishia maumivu makali.

Jana Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kilitoa taarifa ya kulaani ongezeko la matukio hayo na kutoa mifano michache ya matukio ya mfululizo waliotendewa watoto.

Matukio hayo yaliripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari ambayo ni Novemba 11, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ijinga, wilayani Magu, alidaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la sita mwenye umri wa miaka 15. Tukio lingine ni mtoto wa miaka sita, jijini Arusha aliyebakwa hadi kufa Julai, mwaka huu.

Pia, Mtoto wa miaka 12 wilayani Serengeti, aliyebakwa na kujeruhiwa vibaya, huku tukio jingine la mwanafunzi wa miaka 10 kubakwa na mwalimu wake wa miaka 27. Kumeripotiwa pia tukio la mzee wa miaka 60 huko Rukwa kumbaka mtoto wa miaka 10 na visiwani Zanzibar, mzee wa miaka 60 kambaka mtoto wa miaka mitano.

Mfululizo wa matukio haya unapaza sauti kuwa kuna mahali jamii imepotoka kiasi cha kutenda matendo ya kishetani.

Tunajiuliza mtoto wa miaka mitano, 10 au 12, 13 anatamanisha nini kiasi cha babu wa miaka 60 kushindwa kujizuia na kumbaka?

Pia, inatoa taarifa kwa jamii kuwa huenda kuna mahali wazazi au walezi wamekengeuka na kuacha jukumu la msingi la malezi ya watoto wao. Mathalani, maeneo ya mijini tunaona watoto wanaojilea wenyewe au wanalea watoto wenzao, wazazi na walezi wamekuwa na kisingizio cha kutafuta maisha ambayo mwisho wa siku hayana maana yoyote kwa kuwa mtoto ameshaharibiwa.

Lakini inafikirisha sana kwamba wanaume wanaofanya hivi akili zao zinakuwa timamu au? Kuna tatizo gani?

Kijana wa miaka 22 mkoani Lindi alihukumiwa jela miaka 30 kwa kosa la kumbaka mtoto wa shemeji yake, na katika utetezi wake aliomba mahakama kumhurumia kwa kuwa shetani alimpitia.

Kwa msingi huo inadhihirisha lipo tatizo la msingi katika jamii ambalo linahitaji tiba ya wanajamii kuanzia wazee wa kimila, viongozi wa dini, siasa na serikali kushirikiana kuzungumza na jamii mara kwa mara. Ni lazima jamii ichukue hatua kukabili hali hii, watoto wanaharibiwa kisaikolojia na kimaisha, wanapitia wakati mgumu kiasi kwamba baadaye atashindwa kuwa baba na mama mzuri wa kulea binadamu mwingine. Bado kuna kazi kubwa ya kuelimisha jamii inapaswa kufanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali NGOs, kwa kuwa licha ya kuwapo sheria nyingi na kali, lakini bado watu wanajiingiza kutenda matendo maovu dhidi ya binadamu mwingine.

Jitihada nyingi zimefanyika ambazo kwa kiasi kikubwa zilisukuma mabadiliko ya sheria mbalimbali ikiwamo adhabu ya miaka 30 na viboko kwa anayekutwa na makosa hayo, lakini bado NGO, viongozi wa dini na serikali wanapaswa kufanya kazi kwa nguvu zote kuifikia jamii mara kwa mara.

Pia, vyombo vya habari licha ya kuripoti tu bado inatakiwa kwenda mbali na kuwa na mijadala ya kitaifa kwa kukaribisha wataalam mbalimbali. Nchi jirani kunapokwa na jambo linaloisumbua jamii kama mauaji ya wapenzi, basi huitishwa mjadala ambao hukusanya wataalamu mbalimbali na kuzungumza kwa pamoja, mambo ambayo husaidia kusambaza elimu kwa kiasi kikubwa.

Pia, ni muhimu waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi kuchukuliwa hatua, kwa kuwa yapo baadhi ya matukio ya ubakaji na unajisi huhusishwa na imani za kishirikina. Ikiwa waganga watakamatwa na kuunganishwa katika kesi hizo maana yake itasaidia kukabiliana na jambo hilo.

Bila kushirikiana bado matukio haya yataendelea kusumbua jamii na kuwaumiza watoto ambao ndiyo dada, kaka, baba, mama na wazee wa kesho.'

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kadhia za wapigadebe Ubungo isiruhusiwe stendi mpya Mbezi

**STENDI** mpya ya mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani, inayojengwa Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam, inatarajia kufanyiwa majaribio tarehe 25 na kisha kuanza kutumika siku tano baadaye ya mwezi huu, kwa maana ya Novemba 30.

Majaribio na kuanza kutumika rasmi kwa stendi hiyo, kunatokana kukamilika kazi hiyo kwa asilimia 90, hivyo inafungua milango wazi kuchangamkia fursa zinazopatikana kwenye stend hiyo.

Baadhi ya fursa zilizopo mahali hapo zinatajwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, ni fremu za maduka, migahawa, ofisi, huduma za kifedha, duka la kisasa, ofisi za kukata tiketi na hoteli.

Akiwa katika stendi hiyo wiki iliyopita kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi, anasema uwepo wake utaendelea kufungua fursa za maendeleo kwa wakazi wa Wilaya ya Ubungo na anawataka wajiandae kwa hilo.

Kuanza kazi kwa stendi hiyo mpya, itakuwa mwisho wa kutumika stendi ya Ubungo, ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikitumiwa na mabasi yaendayo katika mikoa jirani.

Pamoja na huduma zake, stendi hiyo ya Ubungo inakabiliwa na kero nyingi. Kuna wapiga debe, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakituhumiwa kusumbua abiria na hata wakati mwingine kuwaibia.

Kutokana na kero hiyo, uongozi wa stendi ulishawahi kuomba wadau wote wanaotumia stendi hiyo, kushirikiana kutatua tatizo kero za wapiga debe, kwamba wenye mabasi, abiria na vyombo vya ulinzi ni muhimu.

Jitihada za kuwaondoa wapiga debe katika stendi ni wa muda mrefu, lakini bado wameendelea kuwapo, hali ambayo huenda ikajitokeza hata kwenye stendi mpya ya Mbezi Luis, ikaleta kadhia kwa abiria.

Hivyo, wakati mipango ya kutaka kuzindua stendi hiyo mpya ikiendelea, ni vyema suala hilo la kadhia kwa abiria liliopo Ubungo isiishie huko huko, iliwasiendelee kusumbuliwa

Katika hilo, ni muhimu kukawekwa mipango madhubiti kama vile kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi na kuvipa mbinu mbadala za kukabiliana na wapiga debe, ili wasisogelee stendi hiyo mpya, watafute kazi nyingine halali za kufanya.

Aidha, kuna suala la kuimarishwa mfumo wa ukataji tiketi kwa njia ya kielektroniki, ni jambo muhimu kwa kuwa hatua hiyo itasaidia kuwapunguzia abiria usumbufu ambao wamekuwa wakiupata, wanapokwenda stendi kukata tiketi hizo.

Kutokuwapo kwa mfumo huo, kunawapa nafasi wapiga debe kugombea abiria na kuwapeleka katika mabasi wasiotaka na mwisho wa siku wanaibiwa mizigo yao, lakini kwa mfumo huo, wanaweza kupata tiketi wakiwa nyumbani.

Haipendezi kuendelea kuona wapigadebe wasiovaa sare wakiwapokea abiria na kuwapeleka ofisi za mabasi husika kukata tiketi, ambapo hali hiyo inasababisha abiria wageni wa jiji la Dar es Salaam kuibiwa.

Katika mazingira hayo yakiwamo ya kunyang'anyana abiria, wapo baadhi ya abiria ambao hutapeliwa mizigo yao pamoja na vitu vingine vidogo kama nauli na simu za mikononi.

Ili kero hizo zisijitokeze kwenye stendi mpya ya Mbezi Luis, ni kupiga marufuku wapigadebe kusogelea stendi hiyo, badala yake wawepo watu wanaotambuliwa na mamlaka husika.

Vinginevyo, hata wale waliotangaziwa fursa za kufanya biashara katika stendi hiyo, watakuwa katika hofu ya kuibiwa mali zao, kwa kuwa wapiga debe ni kundi ambalo limekuwa likituhumiwa kujihusisha na vitendo vya wizi.

Stendi mpya ya Mbezi Luis, inatajwa ni muhimu kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hasa katika kuchochea uchumi na biashara.

Matarajio ni kwamba, itachukuwa mabasi 3,456 na kutakuwapo maegesho ya magari ya juu na chini, huku aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Selemani Jafo, alishautaja ni mradi unatoa ajira 600 na kwamba matarajio ya baadaye ni mapato serikalini Sh. bilioni 10 kila mwaka.

Kero zote za Ubungo ni vyema zikashia huko, ili abiria wasikutane nazo tena, kwa kuwa ni aibu hasa kusikia mpiga debe akimsindikiza abiria kwenda kukata tiketi ya basi ambalo anajua halipo, ni bovu ama limeshajaa.

Ndani ya stendi mpya ya Mbezi Luis, abiria waachwe waingie wenyewe kukata tiketi katika mabasi wanayoyataka, badala ya kuwapo kundi la wapigadebe ambao kwa muda mrefu wanalalamikiwa kwa wizi.

# USAID yajivunia kupunguza ujangili Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wa kuendeleza mazingira, uhifadhi na utalii wa Tanzania (PROTECT) limechangia kupunguza ujangili nchini kwa asilimia 80.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni katika kikao cha mtandao kilichorushwa mubashara kusherehekea miaka mitano ya kulinda baioanuai na uchumi unaotokana na utalii Tanzania na taarifa yake kupatikana katika vyombo mbalimbali vya habari nchini.

"Kazi nyingi zilizofanywa na USAID PROTECT zitaacha alama ya kudumu wa uhifadhi Tanzania. Mradi huo umeshirikisha mashirika ya kitaifa na kampuni binafsi zilizopo nchini, ili kupata ushawishi na mali zao katika juhudi za uhifadhi," alisema Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa USAID, V. Kate Somvongsiri, ambaye alifungua kikao mtandao hicho.

"Hii imesababisha kuhifadhiwa kwa zaidi ya hekta 300,000 za maeneo muhimu kibaiolojia na kupunguzwa kwa kiasi kikubwa cha ujangili na uvuvi usiodhibitiwa," alisema. Alisema mradi wa USAID PROTECT uligharimu dola milioni 19.1 na kwamba ulibuniwa katikati ya janga la ujangili lililoshuhudia Tanzania ikipoteza asilimia 60 ya tembo kati ya mwaka 2009 na 2014 pekee.

Somvongsiri alisema ili kushughulikia kwa ufanisi tatizo hilo, mradi huo ulitumia njia ya ubunifu inayojumuisha siyo washirika waliozoeleka wa uhifadhi, lakini Bunge la Tanzania, Mahakama, sekta binafsi na vyombo vya habari.

"Matokeo yake, Tanzania ilijiandaa vyema kupambana na uhalifu wa wanyamapori katika ngazi zote kupitia sera imara za kuzuia uhalifu wa wanyamapori, uelewa mzuri wa jinsi ya kutambua usafirishaji haramu wa wanyamapori na namna ya kuendesha mashtaka na kesi za uhalifu wa wanyamapori," alibainisha.

Kwa kipindi hicho, mradi ulisaidia shughuli mahsusi kama vile programu za mabadilishano ya uzoefu kikanda na mafunzo ya kupambana na uhalifu huu wenye sura mbalimbali na wa kupangwa.

"USAID PROTECT ilishirikiana na Tanzania kuboresha sera za shoroba za wanyamapori kwa kuandaa kanuni za uhifadhi wa maeneo ya mtawanyiko, maeneo ya kingo za maeneo yaliyohifadhiwa na njia za uhamaji, pamoja na mpango kazi wa kutathmini vipaumbele vya shoroba," alisema.

Taarifa hiyo ilisema kuwapo kwa kanuni kutahakikisha shoroba za wanyamapori, maeneo ya mtawanyiko na maeneo ya kingo za maeneo yaliyohifadhiwa yanapatikana, ili kuruhusu wanyama wa porini kutembea kwa uhuru kati ya maeneo yaliyohifadhiwa.

Aidha, ilisema kuwa katika kuandaa wasimamizi wa siku zijazo wa maliasili, USAID PROTECT ilifadhili taasisi tatu za mafunzo ya wanyamapori chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambazo ni Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Afrika - MWEKA, Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori ya Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Jamii cha Likuyu Sekamaganga.

"Kwa kushirikiana na mradi, vyuo viliandaa nyaraka muhimu za taasisi, ikiwa ni pamoja na mipango mikakati, mipango ya biashara na mikakati ya kutafuta fedha. Nyaraka hizi za msingi ni muhimu kuhakikisha mazingira mazuri ya kujifunza ambayo yanaweza kutoa wahifadhi wa baadaye wenye ujuzi, maarifa na wazalendo," alisema.




Mkurugenzi wa Biashara Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa akipunga mikono kuashiria uzinduzi wa huduma ya duka jipya la Vodacom linalotembea katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA, RC wawapa tano walipakodi

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Dk. Edwin Mhede, wamewashukuru wafanyabiashara wa mkoa huo kwa kulipa kodi na kuuwezesha kufikia asilimia 95.6 ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Akifungua mkutano wa masuala ya kodi kati ya wafanyabiashara wa Mkoa wa Iringa na Menejimenti ya TRA, Hapi alisema ni ukweli usiopingika kwamba kutokana na mkoa huo kuwa na shughuli nyingi za kiuchumi, umezalisha walipakodi ambao wamelipa kodi zao kwa mujibu wa sheria.

"Mkoa wetu siyo tu umefanya vizuri katika kodi zinazokusanywa na TRA, lakini hata kwenye kukusanya ushuru wa halmashauri ambao mimi ninausimamia.

"Kwa hiyo, watu wa Iringa ni walipakodi wazuri, kazi hii kubwa imetokana na ushirikiano na taasisi za serikali na wananchi wote wa mkoa huu," Hapi alisifu.

Kiongozi huyo wa mkoa aliitaka TRA kuendelea kutoa elimu ya kodi zaidi kwa makundi mbalimbali ya wafanyabiashara kulingana na aina ya biashara au kodi wanazopaswa kulipa ili kila mwananchi aelewe wajibu wake na kuendelea kuchangia maendeleo ya Mkoa wa Iringa na taifa kwa ujumla.

Awali, Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Mhede, akitoa takwimu za kikodi kwa Mkoa wa Iringa, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20, mkoa huo ulipangiwa kukusanya Sh. bilioni 66.79, lakini ulifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 63.9 ikiwa ni sawa na asilimia 95.6.

"Hiyo siyo hela kidogo, kufikia lengo la juu kabisa pamoja na vikwazo kadhaa ukiwamo ugonjwa wa corona, bado mmefanya vizuri, ninaomba mjione ni watu muhimu na hata mkitoka nje ya Iringa, mseme ninyi ni walipakodi wazuri, tunawashukuru sana," alipongeza Dk. Mhede.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa TRA, Mkoa wa Iringa kwa mwaka huu wa fedha, umepangiwa kukusanya Sh. bilioni 77 kwa kuwa umeonyesha kuwa na walipakodi weledi na wanajua umuhimu wa kulipa kodi kwa taifa lao.

TRA imefanya mkutano na wafanyabiashara wa Mkoa wa Iringa kwa lengo la kuwashukuru walipakodi na wananchi wa mkoa huo kwa kulipa kodi.

Zaidi ya wafanyabiashara 300 mkoani huko walishiriki katika mkutano huo.

# UN yaahidi kutekeleza mradi kusaidia wakimbizi, wananchi

**Na Anthony Kayanda,** KIGOMA

UMOJA wa Mataifa (UN) umeahidi kuendeleza utekelezaji wa miradi ya pamoja Kigoma (Kigoma Joint Program) inayolenga kuwasaidia wakimbizi walioko kambini na wananchi wanaoishi vijiji jirani na kambi hizo.

Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Zlatan Milisic, alisema hayo jana mjini hapa wakati wa kikao cha tathmini kilichoshirikisha viongozi wa serikali na mataifa yanayosaidia wakimbizi.

Miradi huo wa Pamoja Kigoma ulianzishwa mwaka 2017 na utakamilika mwaka 2022 na umelenga kusaidia jamii katika nyanja za kuboresha nishati na mazingira, kuwezesha kiuchumi vikundi vya vijana na wanawake, kuondoa unyanyasaji kwa watoto na wanawake.

Shughuli zingine ni kuboresha elimu kwa wasichana, kuendeleza kilimo cha kisasa na kutafuta masoko ya uhakika, kuimarisha afya bora, kutoe elimu juu ya ugonjwa na ukimwi, kuelimisha juu ya umuhimu wa matumizi ya maji safi na salama ili kuepuka magonjwa ya milipuko.

Milisic alisema ni jukumu la msingi unapoamua kusaidia wakimbizi uhakikishe pia watu wanaoishi jirani na kambi za wakimbizi pia wanapata misaada kwa vile huwa wanaathirika kutokana na uwepo wa wakimbizi.

Amepongeza nchi za Norway, Sweden na Ireland kwa kutoa misaada ya hali na mali kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kikamilifu.

Mkuu wa Mkoa Kigoma, Thobias Andengenye, alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa dhati ili mradi huo ukamilike kwa mafanikio kama ilivyokusudiwa.

Wataalamu na watumishi wa umma wataendelea kusaidia kila nyanja ya mradi huo kwa kuelimisha jamii na wakimbizi ili hata mradi utakapokamilika watu wanufaike na uwepo wa mradi huo.

Ofisa kutoka Ubalozi wa Norway nchini Tanzania, Bjørn Midthun, aliahidi kuwa serikali yake itaendelea kutoa misaada wa fedha katika miradi huo wa kusaidia wakimbizi na jamii inayowaishi kuwazunguka.

Chlóe Horne, kutoka ubalozi wa Ireland nchini, aliwataka wadau kutekeleza mradi huo kikamilifu ili walengwa wanufaike kwa kupata maendeleo katika jamii zao.

Mradi huo unatarajia kugharimu Dola za Kimarekani milioni 63 ambapo hadi sasa kiasi kilichokusanywa kutoka kwa wahisani mbalimbali ni dola milioni 30.6 ukiwa umebakiza miaka miwili kabla ya kukamilika kwake mwaka 2022.

# DPP ateketeza kiwango kikubwa dawa za kulevya

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, amewataka wananchi kutojihusisha na biashara haramu ya dawa ya kulevya na baadala yake watafute kazi zingine za kufanya.

Mkurugenzi alitoa rai hiyo, jana jijini Dar es Salaam wakati wa uteketezaji wa dawa za kulevya zilizopatikana katika kesi mbalimbali zilizotolewa hukumu.

Uteketezaji wa dawa hizo ulihudhuriwa na mawakili wa kujitegemea, majaji, DPP na maofisa wa ofisi yake, maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevya, waandishi wa habari na maofisa mazingira walioshuhudia kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kikiteketezwa.

"Katika shughuli hii tumeteketeza Kg 119.074 za Heroine, Kg 3.93 za Cocaine na Kg 120 za bangi na tunafanya hivyo baada ya kesi ya vielelezo hivyo kumalizika mahakamani," alibainisha DPP Mganga.

Jaji wa Mahakama Kuu, Edwin Kakolaki, aliwataka wananchi kuachana na fikra potofu kwamba vielelezo vivyo huwa havifanywi chochote na serikali.

"Niwatoe hofu wananchi kuwa mara baada ya kesi kumalizika mahakamani, serikali inakuwa na utaratibu wa kuteketeza vielelezo kwa kuchoma moto, hivyo niwatake wananchi kuachana na fikra hizo potofu zinazoenezwa mtaani," alisema.

Kamishna wa Sayansi Jinai Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Bertha Mamuya, aliyataja madhara ya kutumia dawa ya kulevya kuwa ni pamoja na kupata madhara kiafya, kupata matatizo kisaikolojia na kupunguza nguvu kazi ya taifa.



Chifu Richard Luwawo wa Matumbulu, jijini Dodoma akikabidhiwa silaha za jadi mbele ya wananchi wake kuashiria kuanza kutekeleza kazi yake wakati wa hafla ya kumsimika iliyofanyika juzi. **PICHA: ELEUTERI MANGI**

# Kaya maskini zapatiwa msaada wa nyumba

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SHIRIKA la Compassion International Tanzania limetoa msaada wa nyumba 12 kwa kaya zinazoishi katika mazingira magumu kwa Kijiji cha Isongo, Ulanga mkoani Morogoro ili kusaidia watoto wanaolelewa katika familia hizo kuishi kwenye mazingira bora.

Akizungumza wakati wa kukabidhi nyumba hizo juzi, Meneja Mwandamizi wa shirika hilo, Ediwin Mugisha, alisema hatua hiyo imetokana na kubaini changamoto wanazopitia baadhi ya watoto kuishi zaidi ya sita kwenye chumba kimoja.

Mugisha alisema hali hiyo inasababisha watoto hao kushindwa kufikia malengo yao hasa kwa kukosa elimu bora. Alisema hatua hiyo inasababisha kushindwa kujisomea wawapo nyumbani kutokana na msongamano wa watu.

"Shirika letu linajishughulisha na kusaidia kielimu watoto wanaoishi katika mazingira magumu, lakini tulipofika huku tukakuta mazingira magumu zaidi yaani familia moja ya watu sita hadi saba wanaishi katika chumba kimoja, hivyo tukaona tuanze kuwajengea nyumba za kuishi ili wapate fursa ya kuwa katika maisha bora na kuboresha elimu yao," alisema Mugisha

Pamoja na kujenga nyumba hizo, alisema wamejenga madarasa matano ya shule za watoto wadogo ambao wanafadhiliwa na shirika hilo ambao ni zaidi ya 200 wilayani humo.

Mchungaji wa Kanisa la Pentekoste Isongo, Silvanus Mataula, alisema bado kuna uhitaji mkubwa wa watu kujengewa makazi ya kuishi kutokana na kuishi kwenye mazingira hatarishi ili kuwasaidia watoto kukua vizuri. "Sisi kanisa kwa kushirikiana na shirika hili, tumeahidi kuwasaidia hawa watoto katika maeneo yote kuanzia masuala ya elimu, afya na malazi. Kiuhalisia huku vijijini watoto wengi wanaishi katika mazingira hatarishi. Kwa hiyo ni wajibu wa jamii kujitokeza na kuwasaidia ili wafikie malengo yao," alisema Mchungaji Mataula. Nao wanufaika wa nyumba hizo, walielezea kuguswa na msaada huo huku wakisema awali walikuwa wakiishi katika chumba kimoja watu wengi kutokana na ugumu wa maisha, hivyo kulishukuru shirika kwa hatua hiyo.

# Watoto njiti waombea kifurushi NHIF

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Doris Mollel (DMF), inayojishughulisha na kusaidia watoto njiti, imetoa wito kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kuwatambua watoto hao kwa kuwa na kifurushi maalum cha matibabu yao.

Watoto njiti wanazaliwa chini ya wiki 37 na kuhitaji uangalizi maalum pamoja na kupatiwa joto.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Doris Mollel, alitoa ombi hilo jana jijini Dar es Salaam, kuhusu maadhimisho ya siku ya mtoto njiti duniani, inayofanyika Novemba 17 kila mwaka.

Mollel alisema mfuko huo hautoi huduma kwa watoto hao, licha ya kutakiwa kukaa hospitalini kwa zaidi ya miezi mitatu na mama zao, ili waongezeke uzito na kupatiwa dawa maalum.

"Kumlea mtoto njiti ni gharama kubwa, mashine kuwasaidia kupumua hutumia umeme, kuna njiti wanaozaliwa chini ya kilo moja, mashine ya oksijeni moja ya hospitalini ni Sh. milioni 3.5.

"Tunaendelea kuziomba bima kuona namna ya kusaidia kubeba gharama za mtoto njiti, mama anachangia kadi yake ya bima ya afya, akitarajia atajifungua kawaida miezi ikitimia, lakini akijifungua njiti bima haihusiki hapo, mama atahitajika kutoa pesa," alisema.

"Mfano, maziwa Sh. 500,000 hadi 700,000, mashine za joto ni Sh. milioni 3.5 watoto hawa huduma zao ni za mamilioni. Ili kuwa na chumba maalum cha kulea watoto njiti kinahitaji si chini ya Sh. milioni 60," alisema Mollel.

Alisema watoto hao huwa na mahitaji ya vifaa maalum vya kuwasaidia kupumua, dawa za kukomaza mapafu ambazo gharama yake ni kubwa.

"Watoto hawa 'immunity' (kinga ya mwili) yao inakuwa iko chini sababu siku hazikutimia, kukumbwa na maradhi hata baridi ni tatizo kwao, uhitaji maziwa maalum kuwasaidia kuongezeka kilo na mipira ya kupumilia," alisema Mollel.

Pia, alisema, kaulimbiu ya mwaka huu katika siku ya maadhimisho hayo ni 'watoto wanaozaliwa kabla ya wakati, ijali kesho yao' na kwamba taasisi hiyo itatoa elimu kuhusu ukuaji wa watoto hao, kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Hapa nchini kila mwaka, watoto 213,000 huzaliwa njiti wakiwa chini ya wiki 37, kwa kawaida mtoto huzaliwa akiwa kati ya wiki 38 hadi 42.

Watoto njiti 40,000 hufariki dunia kila mwaka, kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo upumuaji.

## HABARI KITAIFA

# 'Jiandaeni kuandika wosia sio uchuro'

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kuachana na dhana kwamba kuandaa na kuacha wosia ni uchuro, wajibu wa kufanya hivyo ni kuepusha migogoro katika familia.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam jana na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Devotha Kamuzora, wakati akiendesha semina ya mirathi na wosia ilioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP). Alisema, jamii ina wajibu wa kuandaa na kuacha wosia ili mtu anapotwaliwa, wanaobaki wahakikishe wanasimamia wosia ama malengo ya marehemu aliyoyaweka kabla ya mauti.

"Kwa vile kila binadamu yupo safarini kuelekea kifo, ni vizuri kujiandaa wakati wa uhai ili akifa aache wanaobaki kuwa salama na kujiepusha na ugomvi na migogoro isiyo ya lazima baina ya wanandugu," alisema Kamuzora.

Alisema, hapo ndipo unakuja umuhimu wa kuandika na kuacha wosia na umuhimu huo unaenda na kufungua shauri la mirathi mapema baada ya kifo cha marehemu. "Kuna wosia wa aina mbili wa mdomo na maandishi, wa maandishi unapaswa kutolewa mbele ya mashahidi wasiopungua wawili; mmoja kutoka katika ukoo/familia na mwingine asiye mwanafamilia na uandikwe kwa kalamu ya wino na si risasi na mashahidi wajue kusoma na kuandika," alisema.

Kwa upande wa wosia wa mdomo, alisema, unaotolewa kwa njia ya kauli na unapaswa kutolewa mbele ya mashahidi wasiopungua wanne. Wawili kati yao wakiwa ni ndugu wa karibu na mtoa wosia.

Kuhusu msimamizi wa mirathi, alisema, anapochaguliwa, anatakiwa kuhakikisha familia iliyoachwa na marehemu haipati shida ama kuadhirika kwa namna yoyote.

Alisema, ni lazima pia msimamizi awe mtu mwaminifu, makini na asiye na upendeleo kwa mrithi ama mfaidika yeyote au mtu mwingine yeyote mwenye nasaba na mirathi hiyo.

Naye mshiriki wa semina hiyo na kiongozi wa kituo cha taarifa na maarifa cha Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Selemani Bishagazi, alisema wapo baadhi ya wasimamizi wa mirathi wanaosumbua wajane. "Unakuta mtu amefiwa na mume wake, lakini msimamizi wa mirathi anaingiza rushwa ya ngono kwa ahadi kwamba anaweza kumsaidia haraka kupata haki yake mahakamani, hii si haki," alisema Bishagazi.

Alisema, amekutana na kesi nyingi za aina hiyo kwenye eneo lake la kazi na kwamba ni vyema kuwa makini katika kuchagua wasimamizi wa mirathi ili kuepusha wajane na kadhia hiyo.

Kwa upande wake Fatuma Mapunda alisema, elimu ya mirathi na wosia inatakiwa kutolewa kwa upana zaidi, kwa kuwa baadhi ya wafiwa wanateseka na kukosa haki kwa kutojua sheria.

Alisema, watu wote hukumbana na matatizo hasa baada ya familia kuondokewa na mmoja wao hasa baba na mama, hivyo elimu zaidi inahitajika ili iwe rahisi watu kuandika wosia.



Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Devotha Kamuzora, akizungumza katika semina kuhusu umuhimu wa mirathi na wosia iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikisha wadau mbalimbali vikiwamo vituo vya taarifa na maarifa vilivyo chini ya mtandao huo, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Daktari atahadharisha jamii magonjwa mlipuko

**Na Saidi Hamdani,** LINDI

KUFUATIA mvua iliyoanza kunyesha sehemu mbalimbali nchini, wananchi mkoani Lindi, wametakiwa kuchukua tahadhari kwa kuyatunza na kuyatumia vizuri mazingira ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Ushauri huo ulitolewa na mtaalamu wa masuala ya afya Hospitali ya Sokoine, Dk. Shadrick Lusasi, katika mahojiano na Nipashe, mjini hapa.

Dk. Lusasi, alisema iwapo wananchi watachukua tahadhari kwa kutunza mazingira na kutumia vyoo bora, jamii itaepuka magonjwa ya milipuko ya kipindupindu na kuhara damu.

Mtaalamu huyo wa afya alisema mvua inaponyesha maji hutiririka maeneo mbalimbali na wakati mwingine husababisha mafuriko yanayosomba uchafu na baadhi ya jamii hutumia mwanya huo kwa kuzibua vyoo na kufungulia majitaka.

"Hii hali inapotokea husababisha vinyesi kusambaa na maji yanapotuama uwepo madimbwi na taka zote hubaki mahali hapo na kuwa kichocheo cha kuzuka kwa magonjwa," alisema Dk. Lusasi.

Alisema katika Manispaa ya Lindi, maeneo mengi kuna visima vya kuchota kwa kutumia kamba na kuwapo uwezekano wa maji yanayotiririka kuingia na kuchanganyika na ya visima.

Alisema mara nyingi utaratibu wa kuzibua vyoo na kuachia majitaka katika kipindi cha mvua na mafuriko hujitokeza maeneo yaliyojengwa bila kufuata mipango miji na wakazi wengi hutumia vyoo vya shimo.

Pia, alisema kutokuwapo kwa miundombinu na utaratibu thabiti wa kuzoa majitaka mitaani, husababisha watu kutafuta njia rahisi ya kuzipunguza, wakijua wanaondoa tatizo kumbe wanahatarisha afya za jamii na za kwao wenyewe, kwa kuwa kipindupindu kinapotokea hakichagui mtu au familia.

Alisema ili kuzuia mlipuko wa magonjwa katika kipindi cha mvua ni vyema jamii wajiepushe na tabia hizo hatarishi, kwa kuhakikisha wanatumia maji yaliyo salama kwa kuyachemsha na kuyachuja kabla ya kuyatumia.

Daktari Lusasi alisema magonjwa yanapojitokeza husababishia hasara kwa serikali na taifa kwa kuwa fedha zilizokuwa zitumike kwa shughuli zingine za maendeleo hulazimika kununulia dawa ili kutibu wananchi wake, hali inayosababisha kupungua kwa nguvu kazi na kutetereka kwa uchumi wa familia na taifa.

Mwanzoni mwa mwaka huu, Kata ya Raha leo, Manispaa ya Lindi, ilikumbwa na mafuriko yaliyosababisha baadhi ya nyumba zilijaa maji na kuharibu mali.

# Tohara yapunguza maambukizi VVU

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UTOAJI wa huduma ya tohara kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 10 na kuendelea wilayani hapa, umesaidia kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) kutoka asilimia 6.4 hadi asilimia 5.3.

Pia, imesaidia kupunguza ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake walio kwenye ndoa, huku wajawazito wakipata elimu ya umuhimu wa tohara wakati wakiwa kliniki na kuwahamasisha waume zao kupata huduma hiyo.

Mratibu wa huduma za tohara, Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Haji Sued, alisema hayo wakati akizungumza na waandisi wa habari, kuwahamasisha wazee, vijana na watu wazima ambao hawajafanyiwa tohara, kufanyiwa.

Sued alisema, huduma ya tohara kwa vijana wenye umri wa kuanzi miaka 10, watu wazima na wazee, imesaidia kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na kipindi cha nyuma yalipokuwa asilimia 6.4.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Mkoa wa Shinyanga ulikuwa juu kwa maambukizi ya VVU kwa asilimia 7.4 na mwaka 2015/2016 yalipungua na kufikia asilimia 5.9 na wanaojitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo ni vijana.

"Kumeibuka uzushi mitaani kwamba tohara inapunguza nguvu za kiume jambo ambalo halina ukweli kabisa...Tohara haipunguzi nguvu za kiume na haiongezi nguvu za kiume wala kuongeza ladha ya mapenzi au kupunguza, ila inamkinga mtu kutopata maambukizi ya Ukimwi kwa asilimia 60 tu," alisema Sued.

Msimamizi wa kitengo cha Tohara Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Damson Samwel, alisema, mwaka 2020 hadi 2021 wanatarajia kutoa huduma hiyo kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 15 na kuendelea zaidi ya 14,000 wilaya nzima.

Vile vile, mwaka 2019 mwezi Oktoba hadi mwaka 2020, walitarajia kuwafikia vijana 6,755, kuwapatia huduma ya tohara na idadi hiyo iliongezeka na kupanga kuwafikia walengwa 14,000.

Aliwapongeza kinamama walio kwenye ndoa kwa kuendelea kuwahamasisha waume zao kufanya tohara kwa ajili ya kujikinga na saratani ya shingo ya mlango wa kizazi na kuwapeleka watoto wao kufanyiwa tohara.

# TRA yasisitiza kodi 10% kwenye nyumba za kupanga

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Nchini (TRA), imewasisitiza wafanyabiashara mkoani Mwanza kukata asimilia 10 ya kodi wanazolipa kwa wenye nyumba wanazopanga kwa ajili ya makazi na sehemu za biashara.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TRA mkoani hapa, Joseph Mtandika, alipozungumza na Nipashe.

Alisema kodi ya aina hiyo inakatwa kutoka kwa wenye nyumba kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya mwaka 2004 na kupelekwa TRA.

Mtandika alisema kila mfanyabiashara mwenye TIN namba ana wajibu wa kukata asilimia 10 kila anapomlipa kodi mwenye nyumba na kuiwasilisha TRA.

Alisema wenye nyumba hawana hiari ya kukataa kodi hiyo kwa sababu inakatwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kwa sasa wanakusanya Sh. milioni 700 hadi Sh. bilioni moja kwa mwaka zinazotokana na kodi za wenye nyumba za kupangisha kwa Jiji la Mwanza.

Mtanda alisema kila mwezi TRA Jiji la Mwanza linakusanya Sh. bilioni 14 hadi 15 kama mapato ya kodi zote.

Alisema kiasi hicho huongezeka au kupungua kutegemea na mwezi husika na wameweka msisitizo kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi.

Kuhusu biashara za magendo kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda kupitia Ziwa Victoria, alisema tatizo hilo limepungua kutokana na mkazo wanaouweka kukabiliana na biashara hizo.

Alisema baada ya nchi za Afrika Mashariki kuweka usawa kwa kodi zinazolipwa, imesaidia kupunguza biashara ya magendo.



Ofisa Mifugo wa Kata ya Mjini, Manispaa ya Shinyanga, Amani Maulidi, akimchoma sindano mbwa, kwenye zoezi la chanjo ya kichaa cha mbwa linaloendelea katika manispaa hiyo, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Magonjwa ya mlipuko yaripotiwa kuongezeka

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAGONJWA ya mlipuko yameripotiwa kuongezeka mkoani hapa baada ya wananchi kupuuza unawaji mikono kutoka wagonjwa 5,092 mwezi Aprili hadi kufikia 6,574 Septemba, mwaka huu.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Ikadi Rashidi, alisema ongezeko hilo limekuja baada ya kutangazwa kupungua kwa kiwango kikubwa cha kasi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid-19) na wananchi kuacha utamaduni wa kunawa mikono kama ilivyokuwa kipindi cha wa ugonjwa huo.

"Kasi ya unawaji mikono hivi sasa imepungua kwa kasi kikubwa sana ikilinganishwa na kipindi kile cha Covid-19 watu walikuwa wananawa zaidi ya mara kumi kwa siku, lakini leo inaweza kupita siku mtu hajanawa na maji ya kutiririka sasa hali hiyo imechangia kuongezeka kwa magonjwa ya mlipuko," alisema.

Alisema, mwezi Januari hadi Machi, mwaka huu, kulikuwa na wagonjwa 7,370 wa mlipuko na mwezi Aprili hadi Juni, mwaka huu, kipindi cha Covid-19, magonjwa ya kuharisha yalipungua hadi wagonjwa 5,092 tofauti ya wagonjwa 2278.

Alisema watu wamepunguza mwamko wa unawaji mikono na kujikuta baadhi yao kula bila kunawa na hivyo kusababisha kupata magonjwa ya mlipuko kama kuharisha kitu ambacho ni hatari kwa afya zao.

Pia, alisema kipindi cha Covid-19 kila nyumba zilikuwa zimetenga ndoo za maji ya kutiririka kwa watu kunawa mikono, lakini hivi sasa utamaduni huo umeanza kutoweka baada ya kuondokana na hofu ya ugonjwa.

Kutokana na ongezeko hilo, Dk. Rashidi aliwataka wananchi wa Manispaa ya Morogoro kuendeleza utamaduni wa unawaji wa mikono ili kupunguza ongezeko la magonjwa ya milipuko pamoja na kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 ambao bado haujatoweka kabisa.

Aliwataka wafanyabiashara wa vyakula na matunda kuweka sehemu zao maji tiririka kwa ajili ya kunawa wateja wao kabla ya kuweka chakula mdomoni na kuweka ndoo za maji chooni na mahali pa kazi.

Kwa upande wake Ofisa Afya wa Manispaa ya Morogoro, Norbert Bilaba, alisema kutokana na ongezeko hilo la magonjwa ya mlipuko, wanakusudia kuanzisha operesheni maalumu ya kupita katika maeneo ya wafanyabiashara wa vyakula, matunda na maduka kuangalia kama wanafuata sheria ya kuweka ndoo za maji na atakayebainika kukiuka hatua kali dhidi yake zitachukuliwa.

# Mbwa 7 wazururaji wapigwa risasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBWA saba wamepigwa risasi katika Manispaa ya Shinyanga kwa kuzurura ovyo na kukosa wasimamizi ili kudhibiti wananchi kung'atwa na kuugua kichaa cha mbwa.

Ofisa Mifugo wa Manispaa ya Shinyanga, Chrispacy Kasimbazi, alibainisha hayo jana wakati wakiendesha operesheni ya kuchanja mbwa, ili kuwapatia kinga ya kichaa cha mbwa.

Alisema katika Manispaa ya Shinyanga kuna idadi kubwa ya mbwa wanaozurura ovyo ambao sasa wanawawekea mitego ili kuwakamata na kuwapiga risasi.

"Natoa wito kwa wamiliki wa mbwa katika Manispaa ya Shinyanga wawazuie kudhurura ovyo mitaani, sisi tukiwakamata tutawatoza faini Sh. 100,000 wakikosa wenyewe tunawapiga risasi," alisema Kasimbazi.

Alisema katika operesheni hiyo wamechanja mbwa 1,143, na wanatarajia kuchanja 2,000 kulingana na dawa waliyonayo na katika manispaa hiyo kuna idadi ya 5,534.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Miti Mirefu, Nasoro Warioba, alipongeza operesheni na kudhibiti kuzurura mitaani, na kwamba alishawahi kumshuhudia mwananchi mmoja aking'atwa na mbwa.

# Ndikilo aonya ubadhirifu korosho

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, ameonya viongozi wa vyama vya ushirika dhidi ya ubadhirifu wa korosho za wakulima.

Alisema hapendi kusikia suala la upotevu wa zao hilo kwa kisingizio cha unyaufu na ikibainika atawashughulikia kukomesha hali hiyo.

Akiongea wakati wa mnada wa kwanza wa korosho aliouzindua juzi katika Wilaya ya Kibiti, Ndikilo alisema hatafumbia macho kiongozi atakayetajwa kuhusika na wizi huo.


Aliwataka wakulima kuanika korosho zao na kuzichambua, kuzipanga kulingana na ubora.

Katika mnada huo wakulima walikubaliana kuuza daraja la kwanza kwa Sh. 2,153.

Said Seif mmoja wa wakulima alisema hawawezi kukubali kuuza daraja la pili kwa Sh. 1,400 ambayo walidai ni ya chini na hailingani na gharama wanazotumia.

Mkuu wa Mkoa alitoa agizo kwa maofisa ushirika kukaa na viongozi wa vyama vya ushirika kupanga kwa pamoja bei na usafiri hadi kufika kwenye maghala ili zisiwe kubwa za kumuumiza mkulima.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji, Shangwe Twamala, alisema mnada huo ulilenga uuzaji wa kilo 2,073,293 sawa na asilimia 55.9 ya korosho zote zilizokusanywa na vyama vya ushirika (AMCOS).



Ukurasa 13

Wananchi wahudumiwe muda wowote, popote



Ukurasa 14

**Ubunifu viwanda nchini sasa waibukia magari ya umeme**

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 13, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Milionea kijana aliyeacha wosia azikwe na gunia la fedha zake

- Alitamba sana kwa 'pamba' nyeupe, sherehe
- Mchango wa mazishi yake umekuwa gumzo

**Na Mwandishi Wetu**

MJUE Genius Kadungure, kijana wa umri miaka 36, yaani mzaliwa wa Oktoba 10, mwaka 1984, ikiwa ni miaka minne na nusu kamili tangu nchi yake kupata uhuru, amefariki dunia akiwa tajiri anayetikisa kitaifa na kimataifa.

Ndiye mfanyabiashara na Mwenyekiti anayemiliki kampuni ya Piko Trading Holdings, mwasisi wa Mfuko uitwao Genius Foundation, hali kadhalika anamiliki klabu ya maarufu ya usiku 'kujirusha' kwa jina Sankayi au maarufu Klabu ya Ndoto za |Maisha ya Usiku (Dreams Nightlife Club).

Darasani nako hajambo, kwani amekanyaga ardhi ya chuo kikuu mara kadhaa, akikwea hadi ngazi ya Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (MBA), kutoka Chuo Kikuu cha Great Zimbabwe, fani aliyoitendea haki katika maisha.

Katika jamii akijulikana zaidi kama Ginimbi, taarifa za msiba wake wa sasa, vyombo vya habari nchini humo sasa vinaripoti ya kuwapo wosia kwamba azikwe na gunia lililojaa fedha na gazeti la Herald linaripoti, mfanyabiashara huyo aliyeishi maisha ya kifahari aliacha wosia huo kwa wanachama wa kikundi cha mazishi kiitwachoi 'All-white Funeral.'

Ginimbi alifariki kutokana na ajali ya gari Jumapili iliyopita, jijini Harare pamoja na mlimbwende Mitchelle Amuli aliyejulikana kama Moana, ambaye familia yake sasa inadai fedha za mazishi kutoka kwa wanaowafariji.

Ginimbi na Maona kwa pamoja walikuwa wanatoka kwenye sherehe ya 'All-white" gari lao lilipogongana na jingine mbele yao, walipochepuka nje ya barabara na kugonga mti kisha kulipuka moto.

Gazeti la Morning Post, linaripoti familia ya tajiri huyo imeahirisha mazishi kwa wiki mbili kusubiri majibu ya utabulisho wa vinasaba (DNA) na kukusanya michango ya kifedha kwa ajili ya kumuaga kwa heshima.





Genius Kadungure 'Ginimbi' katika 'pozi' lake katika zama za uhai wake, pamoja na mandhari ya makazi na sehemu ya mali zake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Matajiri wa Zimbabwe wamekuwa wakiahidi fedha kwa ajili ya mazishi ya Ginimbi, huku mmoja wa manaibu waziri, Tino Machakaire, akiahidi kununua jeneza kubwa kwa ajili ya Ginimbi, Mbunge Temba Mliswa amechangia wanyama wengi kwa ajili ya kuchinjwa kwenye mazishi hayo.

Mwanasiasa, Acie Lumumba, naye ameahidi kutoa lita 1000 za mafuta ya dizeli, kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari vya ndani.

**'PAMBA' NYEUPE**

Ginimbi Genius Kadungure, alijulikana kama Mfalme wa mitindo mbali na kufanya sherehe kubwa .

Mwaka 2010 alifanya sherehe kubwa ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa, wahudhuriaji wakivaa mavazi meupe maarufu kama 'All White Party' jijini Harare Zimbabwe.

Ni sherehe iliyozua gumzo kubwa jijini Harare, huku miaka miwili baadaye, 2012 akaibuka na makuu mengine ya ya siku nyengine ya kuzaliwa kwake.

Mwaka 2013, Ginimbi aligharamia sherehe ya siku tatu katika kijiji cha kwao huko Domboshava, akisherehekea nyumba mpya aliyojenga katika eneo hilo.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa mbalimbali.***

BIASHARA

MKUU UVUVI KAGERA:

# Kagera Tumewekeza mitumbwi elfu nne inayovuna bilioni 3/- na imeajiri 6,900

**Na Lilian Lugakingira,** Bukoba

- Wavuvi: Kweli kuna maendeleo, ila shida nayo ipo!

HALI ya eneo kubwa ya Ziwa Victoria wastani wa robo, kuongeza na makusanyo ya leseni na biashara imekuwa manufaa makubwa katika kukusanyia mapato.

Leo hii Mkoa wa Kagera kupitia Idara ya Uvuvi, imekusanya Sh. bilioni 3.02 zitokanazo katika shughuli mbalimbali za uvuvi zikiwamo leseni na faini, katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Hiyo ni ongezeko zaidi kulinganisha na Sh. bilioni 2.8 zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa lugha rahisi kuna makusanyo ya ziada Sh. milioni 220.

Hayo yanatajwa kuwa matunda ya elimu inayotolewa kwa wavuvi na wafanyabiashara wa samaki.

### OFISA UVUVI

Efrazi Mkama, ni Ofisa Uvuvi wa Mkoa wa Kagera, anasema mbali na elimu iliyotolewa kwa wavuvi, pia walifanya doria zipatazo 199 katika katika mwaka huo wa fedha na kufanikiwa kukamata zana nyingi yo haribifu za uvuvi.

"Yalikamatwa makokoro, timba, mitumbwi na watuhumiwa 137 ambao wamefikishwa katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua mbalimbali ikiwamo faini na kifungo," anasema.

Anasema fedha zinazopatikana ni sehemu ya makusanyo ya ndani ya halmashauri na baadhi zinatekeleza miradi kama ya ujenzi wa mialo ya samaki, kutoa elimu kwa wavuvi na kuboresha mazingira ya kuanika dagaa.

"Fedha nyingine zimetumika kuboresha maeneo ya kupokelea samaki, kujenga maghati ya kuegesha mitumbwi na asilimia kumi imetumika kutoa mikopo kwa vikundi vikiwamo vya vijana na wananchi wengine," anafafanua Ofisa Uvuvi.

Anasema mkoa Kagera una maziwa madogo 11, anayoitaja kwa majina: Burigi, Rwakajunju, Melule, Ruko, Rushwa, Kaburi, Kabindi, Katete na Ikimba.

Pia, Mkama anaeleza kuwa asilimia 27 ya Ziwa Victoria na maji yake yako mkoa humo na anafafanua: "Maeneo haya yanatosha watu kuweka vizimba vya kufugia samaki na kujipatia kipato na kuepuka kushiriki katika vitendo vya uvuvi haramu."

### MAENDELEO YA SAMAKI

Anataja idadi ya mabwawa ya kufuga samaki yameongezeka maradufu, kutoka 624 ya mwaka wa fedha 2018/2019 hadi ziada ya mabwawa 43 katika mwaka 2019/2020, ikifikisha jumla ya mabwawa yaliyopo kuwa 647 na kuwa wanaendelea kuhamasisha wananchi wafuge samaki.

"Wadau mbalimbali wajitokeze katika ufugaji samaki kwa njia za vizimba na mabwawa ya kuchimba, halmashauri zote kwa sasa zimekwishatenga maeneo kwa ajili ya kuwezesha watu kuwekeza" anasema.

Pia, anafafanua serikali imepunguza mlolongo wa utaratibu wa kupata vibali vya kuwekeza kwenye ujenzi wa vizimba na kuwa kwa sasa mchakato wa mtu kupata vibali husika, ni ndani ya mwezi mmoja.

"Kuna wawekezaji watatu wamekwishapatikana kujenga vizimba katika maeneo ya Rubafu na Kemondo Bukoba Vijijini na mwambao wa Ziwa Victoria katika wilaya ya Muleba," anasema.

Mkama analeza hadi sasa serikali inaendelea kutenga maeneo mengine katika nchi kavu na wananchi wameanza kujenga vizimba na mabwawa, baadhi wanaendelea na taratibu za vibali husika.

Anasema, zote ni jitihada zinazolenga kuwezesha uwapo wa samaki wa kutosha, hali anayoamini itapunguza uvuvi haramu katika maziwa madogo yaliyopo ndani ya ziwa kuu - Victoria.



Wavuvi wakiendelea na shughuli zao katika mwalo wa Nyamkazi, katika Manispaa ya Bukoba.

> **Tunafanya ukaguzi na mwaka wa fedha 2019/2020 zimefanyika ukaguzi 166 katika maeneo ya maghala ya samaki, mialo, viwanda, masoko na maeneo mengine ambako shughuli za uvuvi zinafanyika.**



Nyavu haramu zikiteketezwa kwa moto katika ufukwe wa Ziwa Victoria, Bukoba. **PICHA ZOTE: LILIAN SILIMA**

"Wavuvi ambao bado wanafanya vitendo vya uvuvi haramu hasa wa kutumia makokoro, timba, sumu na milipuko nawashauri waache, kufanya hivyo wanaharibu mazalia ya samaki, maeneo samaki wanapoishi na makuzi ya samaki," anasema.

Ofisa Uvuvi huyo wa mkoa, anavitafsiri vitendo vinavyoua samaki wachanga, kuwa ni hatari kwa vizazi vijavyo, akifafanua: "Mfano Sangara ni samaki wa kupandikizwa kwa hiyo wanaweza kuisha kutokana na uvuvi haramu."

Pia, anawataka wananchi kushirikiana na serikali kudhibiti vitendo hivyo, akibebwa kwa kujiona sehemu ya kulinda rasilimali za Ziwa Victoria.

"Uvuvi haramu ukidhibitiwa samaki watapatikana wa kutosha kuuza ndani na nje ya nchi na kuitangaza Tanzania kimataifa," anasema.

Anatumia fursa hiyo kuwaonya wanaotorosha dagaa usiku katika visiwa vya Kerebe na Gozba kwenda nje ya nchi, kwamba watakapokamatwa watachukuliwa hatua, kwa maana ni vitendo vinavyoathiri uchumi wa nchi.

### USAJILI CHAP CHAP

Pia, anasema serikali imeshawasajili wavuvi na mitumbwi yao, lengo ni kuwapo takwimu sahihi na zana zinazotumika na kwa mujibu wa Ofisa Uvuvi huyo kuna jumla ya mitumbwi 4,018.

Hapo na anatoa mgawanyiko uliopo ni kwamba kuna mitumbwi 2,137 inayotumia injini na 1,490 inayotumia kasia.

"Wilaya ya Muleba inaongoza kuwa kuwa na mitumbwi mingi, ambayo ni 1,952 ikifuatiwa na Wilaya ya Bukoba," anasema Mkama.

Anataja kingine kinachofanywa na serikali ziwani ni kudhibiti ubora katika dhamira ya kulinda afya ya mlaji, kwa kuondoa sokoni samaki wasio salama, akitoa mfano waliovuliwa kwa sumu au walioka muda mrefu.

"Tunafanya ukaguzi na mwaka wa fedha 2019/2020 zimefanyika ukaguzi 166 katika maeneo ya maghala ya samaki, mialo, viwanda, masoko na maeneo mengine ambako shughuli za uvuvi zinafanyika," anasema Mkama.

Anasema katika ukaguzi huo samaki wengi walikidhi viwango na kuwa waliokuwa hawafai kwa matumizi ni asilimia ndogo.

### WAVUVI NAO

Lameck Laurean, mvuvi katika mwalo wa Nyamkazi Manispaa ya Bukoba, anasema nyavu za ukubwa wa milimita nane wanazotakiwa kutumia Ziwa Victoria, haziwawezeshi kupata samaki na anaomba waruhusiwe nyavu za ukubwa milimita sita.

"Nyavu tunakatazwa kutumia za 'double' na tunaruhusiwa kutumia za 'single' ambazo ni vigumu kupata samaki, lakini nchi nyingine mfano Uganda wavuvi wanaruhusiwa kutumia 'double' na ziwa ni lile lile," analalamkika.

Mvuvi anayevua eneo hilo, Thadeo Tegamaisho, anasema kwa sasa wanajitahidi kudhibiti uvuvi haramu kutokana na elimu inayoendelea kuwafikia, tofauti walitumia zana tofauti, pasipo kutambua kama ni haramu.

"Kwa sasa maeneo wanayovua kiharamu yamepungua kwa asilimia kubwa, maana hata nyenzo zilizokuwa zikitumika hazipo tena madukani, wakati zamani zilikuwa zikitengenezwa viwandani na ziliuzwa kwa wingi," anaeleza.

Anasema kutokana na wao vijana kukoswa ajira, walijiunga katika makundi kato ya pamoja kama wanne au watano na kununua nyavu hizo haramu kwa lengo la kwenda kuvua kujipatia kipato.

Tegamaisho anakiri sasa, wavuvi wengi wanaogopa kukamtwa na wanatii sheria, akiongeza:"Pia elimu imesaidia kupunguza tatizo."

Kuhusu mikopo ana maoni: "Wanaotoa mikopo wakija hawatufikii sisi wavuvi wenye hali duni, wanawajali wenye mitumbwi tu, wakati wanaopaswa kusaidiwa ni sisi wenye uwezo mdogo."

Anasema kuna wakati wanaambulia mikopo midogo akitaja mfano wastani kati ya Sh. 400,000 na Sh. 500,000, ambayo ni kasi kidogo sana, huku zana kma mtumbwi unafika kati ya Shi.milioni 10 hadi 12.

"Ni bora wachukue wavuvi kama watano ambao watatambuliwa kupitia viongozi wa maeneo wanayoishi, waorodheshwe na kupewa mikopo inayojitosheleza," anasema, akilalamika kuwapo masharti magumu .

"Hivi mvuvi mdogo atapataje leseni wakati hana hata mtumbwi na kipato chake ni cha hali ya chini," anahoji.

Aidha, kuhusu kufuga samaki katika mabwawa, anaomba elimu iwe endelevu kwao, hasa katika namna ya kupandikiza samaki, nayo inahitajika na kuwa wao wanajua kuloa na kutega lakini kupandikiza samaki kwenye mabwawa hawajui.

Kwa mujibu wa Ofisa uvuvi wa Mkoa, sekta hiyo inatoa ajira kwa watu 6,919 mkoani Kagera.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Wananchi wahudumiwe muda wowote, popote






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

HIVI karibuni uongozi wa wilaya ya Temeke chini ya Mkuu wake, Godwin Gondwe, uliandaa wiki ya One Stop Jawabu, ambao idara mbalimbali za serikali zilipiga kambi eneo moja na kuhudumia wananchi waliokuwa na matatizo na kero mbalimbali.

Ilikuwa wiki ya mafanikio makubwa kwa mujibu wa wananchi waliofika eneo hilo na kupata huduma mbalimbali, walizoshindwa kupata huko nyuma walipokuwa wakifuatilia kwenye ofisi za wahusika.

Wapo waliopongeza na kuomba wiki kama hizo ziendelee kuwa zinafanyika, ili kero za wananchi ziondoke sawia. Nami naungana na wananchi kumpongeza Gondwe au Double G kama alivyojulikana akiwa mtangazaji wa ITV.

Napongeza huku nikijiuliza kwa nini mpaka ifanyike hivyo, ndipo wananchi wahudumiwe? Watumishi ni wale wale walioondoka ofisini na majalada yao na kubadili eneo tu, ghafla nyoyo zikabadilika na kuwa na upendo wa kuhudumia wananchi wale wale!

Mtu anaweza kujiuliza maswali mengi, kwa sababu kama serikali imejenga ofisi na kuweka samani na kuwalipa mishahara na posho watumishi hao, iweje mpaka wahamishiwe kwingine ndipo watimize wajibu wao!

Ni jambo la kushangaza. Pengine kunahitajika utafiti wa kisaikolojia na kifilosofia kujua ni kwa nini iliwezekana hiyo kufanyika Temeke na wananchi kuridhishwa na utumishi ule.

Picha inayokuja haraka haraka ni kwamba, pengine watumishi wetu wamezoea kudekezwa au kubembelezwa, kwamba wakiwa ofisini wasihudumie wananchi kwa kuwa hakuna kipimo au tathmini inayofanywa.

Pengine, wakipelekwa viwanjani kwenye mahema na kufuatiliwa kwa karibu kwa imani kwamba mwisho wa utaratibu huo kutafanyika tathmini, basi ndipo watakapochakarika na kuhudumia vizuri wananchi.

Je, inawezekana kwamba kufanyia kazi kwenye mahema kuna bonasi tofauti na kufanyia kazi kwenye ofisi za kawaida? Yawezekana. Lakini huku ni kutowajibika ipasavyo. Ndiyo sababu kabla ya Rais Dk. John Magufuli kuingia madarakani, kulikuwapo na wiki nyingi maalumu katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Ni katika wiki hizo, ndipo watu mbalimbali walifurika wakitarajia kupata huduma za haraka na za papo kwa hapo. Na hilo likifanyika, pia katika maonyesho mbalimbali yakiwamo ya kimataifa ya biashara kwenye viwanja vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Imekuwa ikifanyika hivyo, pia katika maonesho ya kilimo, Nanenane, mikoani, ambako mtu ukienda unahudumiwa haraka tena kwa ukamilifu na kutoka umeridhika, lakini ofisini mara utaambiwa huyu hayupo njoo kesho au hili halipo njoo keshokutwa.

Lakini, kwa matamasha na maonyesho hayo, inaonekana kila kitu kinawezekana katika kuhudumia wananchi wenye shida. Je, tuwe Tanzania ya matamasha na maonesho? Tuwe Tanzania ya wiki maalumu?

Mimi sidhani kama ndio mwelekeo wetu, kwa sababu chini ya kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu, ningetarajia kazi hizo zifanywe kote ili mradi mwananchi anahudumiwa kikamilifu na kuondokana na kero. Hayo ndiyo huwa matamanio ya wengi kutoka serikali wazichaguazo.

Ni bahati mbaya, kwamba Watanzania tunaelekea kuamini katika umaalumu katika kutenda kazi na ndiyo maana kwingineko, Rais Dk. Magufuli amekuwa akikumbana na malalamiko ya watu mbalimbali awapo ziarani.

Kwa kuamini kwamba viongozi hawawezi kuhudumia wananchi pasipo kusukumwa au kushitakiwa, wananchi huandaa mabango na kusimama nayo kwenye mikutano ya hadhara, ili kushitaki au kulalamika.

Awali, Rais alikuwa akifikia mahali na kuyakusanya na kwenda kuyasoma au kusomewa na wasaidizi wake na kuona hatua za kuchukua. Alipoona imekithiri, akatoa maelekezo kwa wawakilishi wake mikoani na wilayani kushughulikia kero za wananchi pasipo kumsubiri yeye.

Hulka hiyo ndiyo pia inazalisha mazoea ya kusubiri matamasha, maonyesho na wiki au siku maalumu katika kutatua kero za wananchi. Hiyo haifai hata kidogo, kwa sababu serikali ipo saa zote na mahali pote katika kusaidia wananchi.

Ni vizuri sana ofisi kutumika kusikiliza wananchi na kutatua kero na matatizo yao kwa wakati, badala ya kusubiri kujengwa mahema viwanjani ndipo fursa za kusikilizwa zipatikane. Huo si uwajibikaji na si utekelezaji wa Hapa Kazi Tu.

UCHUMI

# Ubunifu viwanda nchini sasa waibukia magari ya umeme

• Wawekezaji, wasomi meza moja waja na lao




Ndivyo yalivyo magari ya umeme. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

WASIFU walio nao ni kwamba, Tanzania inaweza kuanza kusikika katika anga za biashara Afrika na kwingineko, kwa sababu tofauti kama baadhi ya mipango inayosukwa nchini hivi sasa, itafaulu.

Ni mradi wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza magari yanayotumia umeme, ambao ni fasheni mpya duniani kote, kutokana na hatari za gesi na matumizi ya mafuta kwa kuongea gesi hatarishi angani.

Kifaa cha msingi katika jitihada hizo ni kutengeneza betri za magari, iwe na mfumo gani, zipatikane kwa bei gani na gari lenyewe liuzwe kwa bei ipi, ili mradi huo uwe endelevu, tafakuri inayotajwa kuendelea huko kwa wachimba madini wa Geita au GGM na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Inahisiwa kuwa tayari GGM imefikia uamuzi ya kuanzisha kiwanda hicho, jambo ambalo kwa mshangao lilitangazwa nchini kutoka Geita na siyo makao makuu ya tawi la kampuni mama ya Barrick Gold jijini Dar es Salaam, inayomiliki kampuni tanzu ya Acacia mwaka jana.

Pia, nia ya kutengeneza magari ya kutumia umeme na hasa betri zake haielekei kuwa umefuatia mazungumzo ya muda mrefu na Chuo Kishiriki cha Uhandisi na Teknolojia (CoET) UDSM, licha ya kuwa kuna uelekeo wa taasisi hizo kushirikiana. Bado kuna maswali kama CoET ni washauri kitaaluma au washirika kimtaji.

> **"Juhudi zinafanyika kuhakikisha kuwa teknolojia zilizopo zinakusanywa, kuzalishwa, kuboreshwa na kutumika kitaaluma kwa ajili ya maendeleo ya taifa.**




Jingine lenye mvuto ni namna Mkoa wa Geita umekuwa na nafasi muhimu katika kuinua wazo hilo na kulifikisha maeneo lilikohitajiwa kujadiliwa, kwani kuna ishara kwamba iwapo mkoa usingekuwa na umuhimu huo tangu mwanzo, ni vigumu kuona namna wangehitaji kuhusishwa mbele ya safari.

Kampuni zikifikia makubaliano yenye umuhimu kitaifa, katika uhalisia wazo la kuunda mradi huo unatosha kutoa tangazo kama hilo, pia inabeba umuhimu kushirikisha uongozi wa nchi.

Msururu wa mambo ya kushangaza kuhusu mradi huo hauishii hapo, kwani GGM wanasema mradi huo unaanza mwakani, ila hapakuwapo ufafanuzi wa haraka kama ni mapema mwakani au baadaye kidogo.

Mambo yaliyo mbele katika ngazi ya utelezaji ni kuandaa majengo yenye miundombinu inayohitajiwa, michoro ya kitaaluma kwa kazi hiyo au malighafi, usanifu na kufanyika upembuzi yakinifu wa gharama, mwelekeo wa mauzo na uwezo uendelevu kibiashara na kimazingira. Majumuisho ya yote, ndiyo yanazaa mipango ya kimkakati hadi utekelezaji kutoka GGM.

Maelezo kuhusu mradi yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel katika jukwa la kibiashara katika Maonyesho ya Madini na Teknolojia ya Geita, akisema mkoa kutiliana saini (wiki hii) na mwekezaji binafsi atakayetekeleza mradi huo.

Taarifa nyingine zilizopsambaa zilimtaja mbunifu huyo na mradi ulivyo na utakayouendeshwa. Hata hivyo, mkuu huyo wa mkoa ndiye aliyefika UDSM kuongea na taasisi hiyo ya ubunifu wa ufundi na utafiti.

Kulikuwapo msisimko wa wazi kwa upande wa Injinia Gabriel, anayesema Geita inataka kuwa kinara 'Bonde la Silicon la Afrika,'sifa ambayo takriban kila kona katika bara la Afrika inapiganiwa, kuanzia Afrika Kusini hadi Nigeria, Misri, Rwanda na kwingineko.

Bonde hilo ni maarufu nchini Marekani, kwa ubunifu na kuanzisha miradi ya 'vichanga' katika teknolojia ambavyo baadaye huwa mashirika makubwa hata yanayotingisha dunia katika fani hizo. Mengi tu ni ya miaka 10 au 20 iliyopita.

Mkuu huyo wa mkoa, anasema juhudi zinafanyika kuhakikisha kuwa teknolojia zilizopo zinakusanywa, kuzalishwa, kuboreshwa na kutumika kitaaluma kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Anadokeza kuwa ndiye angetia saini makubaliano ya kuanzishwa kwa kiwanda cha kuanza kutengeneza magari ya kutumia umeme Jumamosi (iliyopita). Dhamira ni kufanya Geita iwe ya kiteknolojia, kuongezea katika dhahabu.

Mkuu wa Mkoa, anainisha kuwa magari yatakayotengezwa Geita yatakuwa na betri zenye uwezo wa kusafiri umbali wa kilomita 100 kabla ya kuhitaji kujazwa tena, huku akieleza matazamio ya kuwapo magari mawili ya mfano yanayotazamiwa kuwa tayari katika miezi miwili ijayo.

Hadi sasa, mbali na GGM na UDSM (ambayo si kampuni binafsi) kuna kampuni kutoka China, iliyoanzisha mradi wa kituo cha umeme ambacho matumizi ya umeme ya GGM ni muhimu katika mradi huo, kupunguza mzigo kwa gridi ya taifa.

Wakati upana wa mradi huo haujaonyeshwa kikamilifu mbali na kutajwa kwake, mpangilio wake unaonyesha undani wa ubunifu miradi na uwezo wa kujiamini kuhusiana na malighafi, taaluma, mitaji na masoko.

Kuwapo mtaji sahihi tena kwa mji kama Geita, picha yake inaweza kuwa pana kama inawasilishwa katika hafla ya kawaida ya kibiashara na kuwa kielelezo kwamba hatua imefika mbali.



HABARI DODOMA



Wabunge wakimpongeza Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa, baada ya jina lake kupendekezwa na Rais Dk. John Magufuli kuwa Waziri Mkuu, Bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Madiwani 13 wajitosa umeya Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MADIWANI wateule 13 kati ya 56 katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wamechukua fomu kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kugombea umeya na unaibu meya wa jiji.

Akitoa taarifa ya uchukuaji wa fomu za kugombea nafasi hizo jana ofisini kwake, Katibu Msaidizi wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, Said Ngamboi, alisema kati ya madiwani hao 13, wawili ni wanawake.

Ngomboi alisema uchukuaji wa fomu za kuomba kugombea nafasi za meya na naibu meya, dirisha lake lilifunguliwa Novemba 4 na kufungwa Novemba 6, mwaka huu.

Katibu huyo alisema wanachama hao 13 waliochukua fomu, saba kati yao wameomba umeya na sita unaibu meya majina yao yatapitishwa katika mchujo wa chama na mapendekezo yatatolewa kwa majina 3 kwa kila nafasi na kurudishwa kwa ajili ya kupigiwa kura na madiwani wote.

"Majina ya waliogombea mstahiki meya yatapelekwa kuchujwa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM na majina ya wagombea unaibu yatachujwa Halmashari Kuu ya CCM Mkoa wa Dodoma," alisema.

"Kikubwa kwa wale watakaoshinda wanatakiwa kwenda kusimamia ilani ya CCM wakati wakiiongoza halmashauri yetu ya jiji hili," alisema.

Aliwataja waliogombea nafasi hizo kuwa ni pamoja na aliyekuwa Meya wa Baraza lililopita, Prof. Davis Mamfupe, ambaye ni Diwani wa Kata ya Madukani. Wengine na kata zao kwenye mabano ni Gideon Mkama (Hombolo Makulu), Fadhil Chibago (Dodoma Makulu) na Neema Mwaluko (Kilimani).

Pia wamo Loth H. Loth (Ng'ong'ona), David Jackson (Mkonze) na Daudi Mkandi wa Nkuhungu.

Aliwataja waliojitokeza kuchukua fomu ya unaibu meya kuwa ni Jumanne Ngede (Chamwino), Emmanuel Chibago (Matumbulu) ambaye alikuwa naibu meya wa baraza lililopita, Beatrice Ngelangela (Miyuji), Edward Magawa (Ihumwa) na Gombo Kamuli (Ipagala).

Katibu huyo msaidizi aliwataka wagombea wote waliochagulia fomu kwenda kuwatumikia wananchi, huku akitanabaisha kuwa madiwani wa kata za jiji hilo ni 41, huku 15 wakitokana na viti maalumu.

Alisema CCM inatarajia watakaochaguliwa watafanya kazi kwa weledi wakifuata maelekezo yaliyopo kwenye ilani ya chama ambayo imeainisha mambo yote muhimu kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo.

# Wanahabari watakiwa kutafiti na kuandika masuala ya watoto

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, amewataka waandishi wa habari kutafiti na kuainisha masuala mbalimbali yanayohusu watoto ili kujenga jamii yenye mtazamo chanya.

Dk. Jingu alisema hayo jana katika mkutano wake na ujumbe kutoka Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) uliofika ofisini kwake kutambulisha maandalizi ya Tuzo za Waandishi wa Habari kuhusu watoto kwa mwaka 2019 zinazotarajiwa kufanyika Desemba, mwaka huu.

Alisema waandishi wa habari ni muhimu kuandika habari zinazoijenga jamii na kutafuta changamoto zinazowahusu watoto badala ya kujikita katika ukosoaji pekee.

Waandishi wa habari, alisema ni wadau muhimu wa kuleta mabadiliko, hivyo waandike habari zenye majawabu kwenye jamii ili zisilete athari hasa kwa watoto waliofanyiwa ukatili.

"Wakati mwingine mwandishi anaibua tatizo halafu anawaacha hewani kumbe na yeye ni mdau. Anatakiwa kutoa mchango wa kutafuta jawabu, tukiwa na waandishi wenye majawabu watatusaidia sana," alisema.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Deodatus Balile, alisema Tuzo za Waandishi wa Habari hususani Habari za Watoto zinaangalia zaidi uandishi wa habari za watoto wanaokabiliwa na matatizo mbalimbali kwa kushirikiana na serikali ili kupata suluhisho la pamoja kwa ustawi wa jamii nzima.

Katibu wa Jukwaa hilo, Neville Meena, alisema katika maandalizi ya tuzo hizo, watashirikiana na serikali kupitia Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kwa kuwa ndiyo yenye dhamana na masuala ya maendeleo na ustawi wa watoto.

Katika hatua nyingine Dk. Jingu aliwahimiza waandishi wa habari katika maeneo mbalimbali nchini kushiriki kikamilifu katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki ya Mtoto itakayofanyika Desemba 20.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Dunia Salama kwa Kila Mtoto Inawezekana; Chukua Hatua'.

# Elimu yasaidia kupunguza ukatili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ELIMU kupinga ukatili wa kijinsia inayotolewa na serikali kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali, imesaidia kupunguza vitendo vya ukatili nchini, imeelezwa.

Ofisa wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Kituo Kikuu cha Polisi Dodoma, Zawadi Bakari, alibainisha hayo jana alipotembelewa na Shirika la Restless Development linalojishughulisha na maendeleo ya vijana, ikiwamo kutoa elimu ya kupiga vita vitendo vya ukatili nchini.

Alisema hivi sasa jamii imekuwa na mwamko mkubwa wa kuripoti vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara katika jamii.

"Tunashukuru hivi sasa jamii imekuwa na mwamko wa kutoa taarifa pale wanaposikia kuna tukio la ukatili limefanyika. Elimu inayotolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau inawasaidia kwa kiasi kikubwa kutambua haki zao," alisema Zawadi.

Alisema wanalipongeza shirika hilo ambalo linajishughulisha na maendeleo ya vijana nchini kwa kuamua kufanya tathmini ya mwisho ya mradi wa tutimize ahadi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema, kutokana na mashirika hayo kujitoa, jamii inapaswa kuendelea na moyo wa kushirikiana na Jeshi la Polisi Dawati la Jinsia ili kuhakikisha wanatokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mmoja wa vijana waliomo kwenye mradi huo, Amina Mahia, kutoka kata ya Kikuyu Kaskazini jijini hapa, alisema awali katika kata hiyo kulikuwa na matatizo ya vitendo vya ukatili, lakini wametoa elimu ya kutosha kwa jamii katika kukabiliana na vitendo hivyo.

Alisema wanashukuru shirika hilo kuleta mradi huo ambao umeleta matokeo chanya katika maeneo ambayo umetekelezwa.

Johaness Thadeo kutoka Kata ya Chamwino, alisema katika utekelezaji wa mradi huo, waligundua kuwa baadhi ya wanajamii walikuwa wakichukulia kawaida vitendo vya ukatili, lakini kwa sasa elimu wameipata na wanaifanyia kazi.

Alisema jamii hivi sasa imekuwa na mwamko mkubwa wa kutoa taarifa pale wanapoona kuna vitendo vya ukatili vinafanyika.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Sokoine, Kata ya Chamwino, Farida Seki, alisema utekelezaji wa mradi huo umeisaidia jamii kujua namna ya kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya ukatili licha kuwa baadhi watu wamekuwa na changamoto ya kuripoti vitendo vya ukatili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la AFNET, linaloshughulika na Haki za Wanawake, Watoto, Afya ya Uzazi, Jinsia na Utawala Bora, Sara Mwaga, alisema katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia wamekuwa.

Alisema mradi wa 'Tutimize Ahadi' wa miaka mitatu umejikita katika kuwaelimisha vijana juu ya afya ya uzazi, kufuatilia ahadi zilizowekwa na serikali kuhusu lengo la namba tano la maendeleo endelevu.



# HABARI MBEYA



Mtafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Kifyulilo kilichopo Mufindi mkoani Iringa, Issaya Marijani, akitoa maelekezo kwa wataalamu na watafiti wa kilimo wa kituo cha Uyole, kuhusu shughuli wanazofanya katika kuhakikisha wanasambaza teknolojia na elimu ya kilimo bora kwa wakulima, wakati wa kikao kilichofanyika jijini Mbeya jana.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Chalamila awalipua wafanyabiashara wanaokopesha mikopo na riba kubwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema anayo majina sita ya wafanyabiashara wakubwa mkoani hapa, ambao wanafanya biashara ya kukopesha wananchi fedha kinyume cha sheria.

Ameahidi kuyakabidhi majina ya wafanyabiashara hao Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuwachunguza kama wanalipa kodi.

Chalamila aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wafanyakazi wa TRA Mkoa wa Mbeya na kuitaka mamlaka hiyo kuongeza bidii ya kukusanya kodi.

Alisema imezuka tabia ya watu kufanya biashara kubwa bila kufuata sheria ikiwamo kukopesha wananchi fedha kwa kuwatoza riba kubwa isiyoendena na miongozo ya serikali. "Kuna watu wanakopesha wananchi kiasi kukubwa cha fedha kinachofikia mpaka Sh. milioni 500. Wanatoza riba kubwa, lakini hawana kibali cha kufanya biashara hiyo na wala hawalipi kodi kulingana na biashara wanayoifanya," alisema.

Chalamila aliitaka TRA kuanza uchunguzi na kuwabaini watu wanaofanya biashara hiyo na kufuatilia kama wanalipa kodi kwa mujibu wa sheria, huku akisema atawapatia majina sita ya kuanzia uchunguzi wao.

"Hapa nina majina sita ya watu wanaofanya biashara ya kukopesha fedha bila kibali cha biashara hiyo, majina haya nitakupatia Meneja wa TRA ili muwachunguze na kuangalia uhalali wa biashara yao na kama hawakwepi kodi," alisema Chalamila.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema TRA inao wajibu wa kisheria wa kufuatilia kila aina ya biashara inayofanyika na kujua uhalali wake, ili kukusanya vizuri kodi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Eunice Liheruka, alisema mamlaka yake imepokea maelekezo hayo na kuahidi kuyatekeleza kwa kiwango cha juu.

"Tumepokea maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na kwa niaba ya wafanyakazi wa TRA Mkoa wa Mbeya. Naahidi kuwa tutayatekeleza yote kwa kasi na kwa kuzingatia sheria za nchi," alisema Liheruka.

Mkuu huyo wa Mkoa pia aliipongeza TRA Mkoa wa Mbeya kwa kuvuka lengo la makusanyo ya kodi katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2020/21. Katika kipindi hicho, mamlaka hiyo imekusanya asilimia 101 ya lengo lililowekwa.

## Neema ya maji yawashukia wananchi Kyela

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI wilayani Kyela imewahakikishia wananchi kuboresha miundombinu ya maji, ili wapate huduma hiyo kwa urahisi na kwa gharama nafuu na kusaidia kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta, aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye ziara ya kukagua vyanzo mbalimbali vya maji yanayotumika wilayani humo ambavyo vingi vinapatikana katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

Alisema serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Kyela fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi mingi na kwamba baadhi ya miradi hiyo imekamilika na mingine iko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Kitta alisema ili miradi inayotekelezwa na serikali iwe na faida kwa wananchi na idumu kwa muda mrefu, ni lazima kila mwananchi ashiriki kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji ikiwamo kutokata miti kwenye vyanzo hivyo.

"Tuna miradi mingi sana ambayo asilimia kubwa ya vyanzo vyake viko Busokelo. Sasa ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunavitunza vyanzo hivi kwa kuvitembelea mara kwa mara ili tuwe na uhakika wa kupata maji muda wote," alisema Kitta.

Alizitaka jumuiya za watumia maji wilayani humo kuhakikisha zinakusanya mapato ya kutosha matengenezo ya baadhi ya vifaa kwenye miradi hiyo yawe yanafanyika mara kwa mara.

Baadhi ya wananchi, waliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maji ambayo waliahidiwa kwa madai kuwa kwa sasa huduma hiyo ipo kwa kiwango kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa hawana uhakika wa huduma hiyo.

Joseph Mwakifuna, mkazi wa Mji wa Ipinda, alisema awali walikuwa wanategemea sana maji ya kwenye visima ambayo usalama wake ni mdogo kwa afya zao, lakini sasa hivi wanatumia majisafi ya bomba.

Alisema kabla ya maji ya bomba kuanza kutumika, mara nyingi wananchi walikuwa wanaumwa matumbo na kukumbwa na kipindupindu ulikuwa unawasumbua hasa kipindi cha mvua ambapo maji machafu yalikuwa yanaingia kwenye visima.

"Sasa hivi maji ya visima tunayatumia kwa ajili ya kufulia nguo na kuoga, hakuna tena kunywa kwa sababu tuna majisafi ya mabomba na tunahamasishwa kila mwenye uwezo avute bomba nyumbani kwake," alisema Mwakifuna.

Alisema hata katika Kituo cha Afya cha Ipinda ambacho ni miongoni mwa vituo bora vya afya katika mkoa wa Mbeya, maji yalikuwa tatizo kubwa awali lakini kwa sasa yapo ya kutosha.

Mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alifanya ziara ya kukagua miradi ya maji katika wilaya hiyo na alizindua mradi wa maji wa Kapapa Group ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.5.

Mradi huo unaanzia katika chanzo kilichopo Busokelo wilayani Rungwe na unahudumia zaidi ya wananchi 13,000 wa vijiji nane kutoka katika Kata ya Ipinda, Mwaya, Talatala na Ikama.

## Wakumbushwa kuhusu sheria

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MADEREVA wa bajaji katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamekumbushwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kukabiliana na ajali za barabarani na matukio mengine yanayogharimu maisha ya watu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema hayo jana kwenye kikao kilichowahusisha madereva na wamiliki wa bajaji, Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na Jeshi la Polisi kwa lengo la kujadili vikwazo wanavyokabiliana navyo waendesha bajaji pamoja na vitendo vya uhalifu.

Matei alisema bajaji zinaweza kuchangia vitendo vya uhalifu kwa sababu zinabeba watu wa aina mbalimbali, hivyo madereva wanapaswa kuwa makini kwa kuhakikisha wanapohisi watu wasio wa kawaida watoe taarifa kwenye vyombo vya usalama.

"Nawakumbusha madereva wote kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za usalama barabarani kwa kuhakikisha mnaepuka ajali na matukio ya uhalifu," alisema.

Mwenyekiti wa Madereva wa Bajaji katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Iddi Kasangula, alisema madereva wengi wa bajaji wamekuwa wakikamatwa na TARURA kwa madai kuwa wanapaki katika maeneo yaliyopigwa marufuku sambamba na kudaiwa kutolipa ushuru.


Kuhusu uhalifu, Kasangula alisema mara nyingi hufanyika majira ya usiku ambapo baadhi ya madereva ambao wengi ni (deiwaka) hubeba wahalifu kwa kutokujua au wengine hushirikiana nao kutekeleza vitendo hivyo.

Kutokana na sababu hizo aliahidi kushirikiana na Jeshi la Polisi kuripoti vitendo hivyo pamoja na kuwaambia madereva wote kutofumbia matukio hayo pindi wanapoyaona.

Mwakilishi wa TARURA jijini Mbeya, Akalu Nyari, alisema suala la ushuru ni la kizalendo kwa sababu kupitia fedha hizo maendeleo yanapatikana ndani ya jamii ikiwamo ujenzi wa shule, hospitali, maji na huduma nyingine muhimu.

Hivyo alidai madereva bajaji wataendelea kulipa ushuru na kuongeza kuwa suala la kukamatwa kwa bajaji zinazopaki kwenye maeneo yaliyopigwa marufuku litaendelea ili liwe fundisho kwa wengine.

Madereva wa bajaji walieleza vikwazo vinavyowakabili wawapo barabarani kuwa ni ufinyu na ubovu wa barabara zilizopo katikati ya mji na kusababisha foleni.



# TAMWA yampa neno Mwinyi kuhusu uteuzi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimemwomba Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuangalia usawa wa kijinsia katika kuunda safu ya uongozi kwenye ngazi mbalimbali.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema Rais ameshamchagua Makamu wa Pili wa Rais na Mwanasheria Mkuu, hivyo kufanya utawala wa juu kuwa unashikiliwa na wanaume pekee.

Dk. Mzuri alisema Zanzibar ikiwa sehemu ya Tanzania, ina jukumu la kufikia usawa wa kijinsia katika vyombo vya uamuzi kama mikataba ya kimataifa na ya kikanda inavyoeleza.

"Zanzibar pia inatekeleza mipango mbalimbali ya nchi ikiwamo kupunguza umaskini, sera ya utawala bora, Mpango wa Kitaifa wa Kupunguza Ukatili wa Kijinsia ambayo inasisitiza usawa wa kijinsia na uwakilishi katika vyombo vya uamuzi," alisema Dk. Mzuri.

Alisema ni jambo jema Dk. Mwinyi katika vipaumbele vyake, amesisitiza kupambana na ukatili wa kijinsia, hivyo ni muhimu kuchagua wanawake katika uongozi ikiwa njia mojawapo ya kupunguza ukatili na kuongeza sauti zao katika vyombo muhimu vya uamuzi.

Katika awamu iliyopita, alisema Zanzibar ilikuwa na mawaziri wanawake watano kati ya 17, sawa na asilimia 29 na kulikuwa na makatibu wakuu wanawake wanne kati ya 15 ambao ni sawa na asilimia 26.

Alisema ni vyema Dk. Mwinyi akaendelea kuteua wanawake ili pengo hilo la usawa liondoke hasa ikizingatiwa kuwa wanawake wanazidi wanaume kwa idadi nchini kwa mujibu wa sensa.

"Ni jambo la fahari kuwa katika uchaguzi uliopita wanawake wengi wamejitokeza kupiga kura na pia kugombea katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Zaidi ya wanawake 435 wamegombea katika uchaguzi wa ushindani ikiwamo uwakilishi, ubunge na udiwani kupitia vyama mbalimbali vya siasa," alisema.

Pia alisema wanawake waligombea kupitia viti maalum, hivyo inaonyesha ni jinsi gani wanawake walivyo na tunu ya kushiriki katika uamuzi ili kupanua changamoto mbalimbali za kijamii na za kwao binafsi.



Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji (wa pili kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Mhazini wa Benki ya NMB, Aziz Chacha, alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye viwanja vya Baraza la Wawakilishi Zanzibar jana. Benki hiyo, inatoa ushauri, elimu na huduma za kibenki kwa wajumbe wa baraza hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ... Mwenyewe aahidi kuwasaidia wajane

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema atahakikisha anawasaidia wanawake wajane kwa sababu wananyimwa haki zao ikiwamo suala la mirathi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati akilifungua Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje kidogo ya Mji wa Zanzibar.

Alisema wajane wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo baadhi yao kudhulumiwa mirathi hasa pale waume zao wanapofariki dunia.

Baadhi yao, alisema wamekuwa wakitelekezwa na watoto na kuachiwa mzigo mkubwa wa malezi kwa watoto wao bila ya kuwa na msaada kutoka kwa familia za baba wa watoto wao.

Alisema wajane hao huachiwa mzigo wa malezi ya watoto hasa ndoa itapovunjika ambapo baadhi ya wanaume hukwepa majukumu ya kuwahudumia watoto au mume anapofariki huachiwa na watoto.

"Nawapongeza wajane wa Zanzibar kwa kuanzisha jumuiya yao ambapo itakuwa rahisi kuwasaidia," alisema.Kutokana na ahadi hiyo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wajane Zanzibar, Tabia Makame, alimpongeza kiongozi huyo kwamba kauli yake hiyo italeta neema kwao. "Hotuba ya Rais inadhihirisha wazi na msemo wake usemao yajayo yanafurahisha, hivyo tuna imani kuwa na sisi wajane tutafurahi kwani ameahidi kusimamia haki zetu," alisema.

Pia alikemea tabia ya utoaji holela wa talaka na kwamba wako baadhi ya wanawake wapewa talaka kwa sababu ya kushiriki katika siasa. "Wako wanawake waliopewa talaka na waume zao kwa sababu ya kushiriki katika siasa na uchaguzi mkuu uliopita wakati kupiga kura ni haki ya kikatiba na kidemokrasia," alisema mwenyekiti huyo. Meneja Mradi wa Jumuiya hiyo, Khamis Ali Rashid, alimpongeza Rais Mwinyi kutokana na hotuba yake hiyo na kumtakia mafanikio mema katika uongozi wake.

"Ni faraja kubwa sana kwa taasisi yetu kutajwa vyema na Rais kwenye hotuba yake ya kwanza kabisa ya kufungua Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Tunaamini kwamba hii haikuwa rahisi bali kazi ilifanyika kwa misingi hii tunaahidi kuendelea na kazi kwa bidii, uaminifu na uadilifu mkubwa," alisema.

# Watengeneza sabuni walia ukosefu wa soko

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wanaotengeneza sabuni za maji wamesema baada ya kuondoka kwa janga la corona, wananchi wamerejea utamaduni wao wa kutonawa mikono kwa maji na sabuni hali ambayo imesababisha kukosa soko.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa wajasiriamali hao, Hidaya Abdallah, alisema soko la bidhaa zao hivi sasa limekuwa na changamoto nyingi ikiwamo kukosa wateja.

Hidaya alisema wakati nchi ikikabiliwa na janga la corona soko la sabuni ya maji lilikuwa zuri hali ambayo ilipelekea kuzalisha sabuni kwa wingi.

"Hivi sasa jamii haina utamaduni wa kuosha mikono kwa maji na sabuni na hata katika baadhi ya taasisi na ofisi mbalimbali zilizokuwa zinatumia sabuni kwa ajili ya kuosha mikono hivi sasa wameacha kabisa," alisema.

Licha ya corona kumalizika, alisema uhamasishaji wa kunawa mikono kwa maji na sabuni hauna budi kuendelezwa ili kuepukana na maradhi mengine ya kuambukiza.

Pia alisema licha ya soko la sabuni kushuka, kuna changamoto ya kukosekana kwa vifungashio vya kuhifadhia sabuni za maji.

"Hivi sasa vifungashio vimeadimika hasa chupa za 'kupres' ambazo ni nzuri zaidi kwa kuhifadhia sabuni ya maji," alisema.

Naye Ofisa Uwezeshaji kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, ambaye anasimamia Mradi wa Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi (WEZA), alisema TAMWA inatarajia kurejesha soko la wazi kwa wajasiriamali ili kuuza bidhaa zao.

Alisema soko hilo lilikuwa likifanyika kila mwisho wa mwezi, lakini lilisimama baada ya nchi kukumbwa na corona.

"Hivi sasa tunatarajia kulirejesha soko la wazi la wajasiriamali ili kuuza bidhaa zao," alisema Nairat.

Aidha, aliwataka wajasiriamali kutovunjika moyo kutokana na changamoto zinazowakabili na badala yake kuongeza udhalishaji wa bidhaa zao na kuzitangaza ili zinunuliwe.

Ofisa huyo alikiri kuwa soko la sabuni ya maji limepungua baada ya corona kumalizika nchi tofauti na kipindi cha corona ambapo mahitaji ya sabuni hizo yalikuwa makubwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

*NIPASHE NI JIBU LAKO*
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA KWA VYETI



**WILLIAM NASHON KENNEDY** anatangaza kupotelewa na vyeti. Cheti namba **S/No. BCD 00450** kilichotolewa na Chuo cha Bandari Januari 13, 2020. Cheti namba **S/No. BCD 01306** kilichotolewa na Chuo cha Bandari Februari 24, 2020. Cheti namba **S/No. BCD 02197** kilichotolewa na Chuo cha Bandari Februari 11, 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MS/RB/2157/2020.**

115994702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NDUGU LEMBURISI LUCAS** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T950 AHY** ENGINE NO **.121514445** CHASSSIS NO. 5ALLON.TEA.**124809** LANDROVER

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**TAARIFA: USR/TR/RB/440/2019.**

115995502

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FLORAH STEPHEN MOSHI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 366 ACG.** Chassis namba **LKIPCKLI7C1078648.** Engine namba **162FMJ420405766.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **BNG/RB/86/2020.**

115995402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI–MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;336/2020**

**Ombi la MBWANA KHALID MBWANA, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMISI KHALID MBWANA .**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 15/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakama-ni waweza kukaguliwa tarehe 05/11/2020.

115995602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**

**SHAURI LA MIRATHI NA 12/2020**

**Maombi ya harua za usimamizi wa Mirathi ya CALVIN AITAEL MAIMU...MAREHEMU**
**NA**
**1.PENIEL AITAEL MAIMU**
**2.RAYMOND CALVIN MAIMU**
**3.AMIN WERAIKIO LEMA.............WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75 na 76)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi ya mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 14 mwezi 12,2020.
**Imewasilishwa leo tarehe 9.Mwezi 11,2020**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

115995902

## KUPOTELEWA KWA VYETI



**WILLIAM NASHON KENNEDY,** Amepotelewa na vyeti vifuatavyo ,cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 1226-0119** kilichotolewa na shule ya secondary BUKWE mwaka 2010,cheti cha udereva VETA(DAR ES SALAAM) **No 167373** mwaka 2019, cheti cha computer VETA (DAR ES SALAAM) **No 163888** mwaka 2019, na cheti cha EXVATOR OPERATING kilichotolewa na VETA (SHINYANGA) **No 194236** mwaka 2020, yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **MIS/RB/2157/2020**

115994702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ROGACIAS MASAWE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 994 ANN SANLG.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MEA/RB/123/2016.**

115995102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EDWARD EMMANUEL MGINA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SUZUKI ESCUDO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 428 AGL.** Chassis namba **TAOIW849060.** Engine **G16A2433685.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/394252/2020.**

115995002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi 2020**

**Ombi la JULIUS GIDION MTOI kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu ALOYCE GIDION MTOI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 20/11/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 10/11/2020

HAKIMU
MAKOLE
DODOMA

115994502

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**CEDRICK DEUSDEUT MBUNDA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 241 ABB.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CEN/RB/2716/2020.**

115995302

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JUVENALIS ERNEST BARAKA** anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki aina ya **XL 125 HONDA,** yenye chasses number **L125S-5736132** na namba za usajili **MC 577 AXB,** iliyosajiliwa na World Vision Tanzania. Kadi hii ilipotea **03/08/2020** ikiwa kwenye bahasha.
Imetolewa taarifa polisi na kupata RB numba **KAG/BUK/RB/793089/2020**
Yeyote atakayeiona aipeleke kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

115995202

**OFISI ZA MATANGAZO**
***Mikocheni Industial Area,***
***Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mob: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***website: www.ippmedia.com***

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Rais, wabunge waondolewa kinga ya kushtakiwa

**ADDISABABA,** Ethiopia

BUNGE la Ethiopia limewaondolea kinga ya kushtakiwa wabunge 39 akiwamo Rais wa jimbo la Tigray, Debretsion Gebremicheal.

Hatua hiyo inakuja wakati mgogoro ukiendelea katika jimbo la Tigray.

Vyombo vya habari nchini Ethiopia vimeripoti juu ya hatua hiyo ya bunge kwamba miongoni mwa walioondolewa kinga hiyo ya kutoshtakiwa yumo pia, Getachew Reda, ambaye ni Ofisa Mwandamizi wa kundi la ukombozi wa watu wa Tigray TPLF ambalo liko katika mapambano na vikosi vya jeshi la serikali kuu.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, alisema operesheni hiyo ya kijeshi imeikomboa sehemu ya Magharibi ya jimbo hilo la Tigray, ambako wanajeshi wa serikali wamekuwa wakipambana na wanajeshi wa jimbo hilo kwa wiki nzima sasa.

Umoja wa Mataifa (UN), umeelezea wasiwasi wake kuhusu mgogoro huo wa Tigray na athari zake kwa wananchi.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa UN, Antonio Gutterres, Stephanie Dujarric, alisema umoja huo unaendelea kutafuta ufumbuzi wa kuwalinda raia.

"UNHCR imetuambia wanashirikiana na mamlaka nchini Sudan kuwasaidia wakimbizi zaidi ya 7,000 waliokimbia kutoka Ethiopia katika kipindi cha siku mbili zilizopita," alisema Dujarric na kuongeza:

"Bila shaka hii ni kutokana na mapigano ya Tigray. UNHCR na maofisa wa huko wanakagua na kuwaandikisha watu wanaowasili Sudan. Wakimbizi wengi kutoka Ethiopia wanatarajiwa kuwasili katika nchi za jirani," alisema Dujarric.

Kadhalika, Mkuu wa Shirika la UN la misaada ya kibinadamu nchini Ethiopia, Sajjad Mohammed Sajid, alisema zaidi ya raia 1,000 wa nchi mbali mbali za kigeni wamekwama katika jimbo hilo la Tigray. **DW**

# Kenya yakataa NHIF kugharamia matibabu Corona

**NAIROBI,** Kenya

SERIKALI ya Kenya imesema haiwezi kugharamia matibabu kwa wagonjwa wa Corona nchini humo, kupitia bima ya afya ya NHIF kwa sababu matibabu hayo ni ghali sana.

Raia wa Kenya mwenye bima ya NHIF hulipia kila mwezi mfuko huo, ili kugharamia matibabu mbalimbali yakiwamo ya dharura.

Hatua hiyo inajiri wakati Kenya inapambana na wimbi la pili la maambukizi ya virusi vya Corona, idadi ya watu wanaoambukizwa ikiendelea kuongezeka kila siku.

Waziri wa Afya, Mutahi Kagwe, aliiambia Kamati ya Bunge ya Afya kwamba matibabu ya Corona ni ghali sana, kwamba serikali haiwezi kumudu kugharamikia katika hospitali za umma au za kibinafsi.

**Kwa kawaida, serikali huwa haigharamii matibabu kutokana na magonjwa kama janga la corona kwa sababu utakuwa mzigo mkubwa kwa serikali.**

"Tuna bahati kuwa matukio mengi tuliyonayo yanahusu watu walio na mifumo ya bima ya afya ya kibinafsi, kampuni hizo zinawafaidi. Lakini linapokuwa suala la magonjwa ya kawaida, serikali kupitia NHIF itatekeleza wajibu wake. Kisha serikali inaweza kuongeza mfuko huo," Alisema Kagwe.

Kwa kawaida, serikali hulipia gharama kwa wote waliojiunga na wanalipia kila mwezi kuwawezesha mwananchi kufikia huduma maalum za matibabu kote nchini katika hospitali za umma na za binafsi.


NHIF pia hugharamia mahitaji ya matibabu ya ghafla na huwa nafuu kwa wagonjwa wenye kipato cha chini.

Serikali ya Kenya imesema kuwa kila mkenya atakayeugua corona, atagharamia matibabu yake.

Kagwe alisema kwa kawaida, serikali huwa haigharamii matibabu kutokana na magonjwa kama janga la corona kwa sababu utakuwa mzigo mkubwa kwa serikali.

Kwa sasa, inagharimu Dola za Marekani 100 kupima virusi vya Corona, kila mtu. Gharama hiyo imesababisha Wakenya wengi kukosa kujipima na kutambua iwapo wameambukizwa virusi hivyo.

Wakenya wameishutumu serikali kutokana na hatua hiyo. Wameikashifu serikali kupitia mitandao ya kijamii wakisema haijali kabisa raia wake wanaofanya kazi kwa bidii kila siku kujenga uchumi wa nchi hiyo. **VOA**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres. **PICHA: UN**

# Walibya wakubaliana kuandaa uchaguzi

**TRIPOL,** Libya

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema Walibya wanaoshiriki katika mazungumzo yanayosimamiwa na umoja huo, wamekubaliana kuhusu mpango wa awali wa kuandaa uchaguzi katika kipindi cha miezi 18 ijayo.

Mazungumzo hayo yanayosimamiwa na UN yanafanyika Gammarth, Tunisia, wakati juhudi za kidiplomasia zikiongezeka, ili kuvimaliza vita vilivyodumu kwa karibu muongo mmoja kwenye nchi hiyo ya Afrika Kaskazini.

Kaimu Mjumbe Maalum wa UN kuhusu Libya, Stephanie Williams, alisema kuwa wajumbe wa pande zinazohusika na mzozo wa Libya wamefikia makubaliano hayo na kuweka wazi hatua za kufanyika kwa uchaguzi mkuu, ikiwamo makubaliano ya kimsingi ya katiba.

"Leo washiriki wa mazungumzo ya kisiasa ya Libya, wamefikia makubaliano ya awali ya kumaliza kipindi cha mpito na kuandaa uchaguzi wa rais na wabunge utakaokuwa huru na haki, utakaozijumuisha pande zote na utakaokuwa wa kuaminika," alisema Williams.

Mazungumzo hayo yanalenga kuanzisha mfumo na serikali ya muda itakayoandaa uchaguzi pamoja na kutoa huduma katika nchi hiyo iliyoharibiwa na vita vya miaka mingi, pamoja na kuathiriwa na janga la virusi vya corona.

Williams alisisitiza kuhusu umuhimu wa kuingia haraka kwenye uchaguzi wa kitaifa ambao utakuwa huru na utakaozingatia uhuru wa kujieleza na haki ya kukusanyika.

Mazungumzo hayo ya Tunisia yanafanyika sambamba na mazungumzo ya kijeshi ndani ya Libya kwa lengo la kujaza taarifa za makubaliano ya kihistoria ya kusitisha mapigano yaliyofikiwa Oktoba, mwaka huu.

UN uliwachagua wajumbe 75 kushiriki katika mazungumzo hayo ya kisiasa, ili kuziwakilisha taasisi zilizopo na jamii za watu tofauti wa Libya, hatua iliyozusha ukosoaji mkubwa kuhusu mchakato huo na uaminifu wake.

Hata hivyo, makubaliano hayo yaliyofikiwa siku ya Jumatano, yaligubikwa na kuuawa kwa kupigwa risasi wakili maarufu na mtetezi wa haki za wanawake katika mji wa Benghazi ulioko mashariki mwa Libya, siku moja kabla.

Hanan al-Barassi, mkosoaji mkubwa wa ufisadi, matumizi mabaya ya madaraka na unyanyasaji dhidi ya wanawake, aliuawa mchana na mwanaume mwenye silaha.

Akizungumzia mauaji hayo, Kaimu Mwakilishi wa UN nchini Libya, Stephanie Williams, alisema yanaashiria kitisho wanachokabiliana nacho wanawake wa Libya wakati ambapo wanasimama kutetea haki.

Williams alitaka haki itendeke na wauaji wa Al-Barassi wafikishwe katika vyombo vya sheria, ingawa alikataa kutoa maoni yake iwapo mauaji hayo yanahusika na mazungumzo yanayoendelea.

Alisema kutakuwa na vikwazo, kutakuwa na watu wasiotaka mabadiliko, lakini Walibya wengi wana hamu kubwa ya kurudisha enzi ya utawala halali wa taasisi zao. **DW**

# BATSHUAYI KUPELEKA KIWANGO CHAKE EPL




**BRUSLLES,** Ubelgiji

STRAIKA wa Ubelgiji, Michy Batshuayi, anataka kiwango alichokionyesha kwa kikosi cha timu ya taifa kukihamishia kwenye klabu yake baada ya mechi za kimataifa.

Batshuayi alifunga mabao yote mawili wakati Ubelgiji wakiibuka na ushindi wa 2-1 kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Uswisi, juzi Jumatano.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 sasa amefikisha mabao 21 kwa Ubelgiji, huku matano akifunga kwenye mechi zake tatu zilizopita.

Hata hivyo, habari imekuwa tofauti kwa Batshuayi kwenye Ligi Kuu England, ambapo anacheza kwa mkopo kule Crystal Palace akitokea Chelsea, bado hajaweza kufunga katika mechi tano msimu huu.

"Kwanini nafunga kirahisi sasa hapa? Hilo ni swali ninajiuliza mimi mwenyewe," amesema Batshuayi akiiambia RTL Sport.

"Inatia hasira, lakini sifikirii kuhusu yaliyopita, nasonga mbele. Binafsi najisikia vizuri kufunga mabao mawili hapa.

"Inaonyesha kwamba nina ubora, natakiwa kujaribu kuwa na kiwango kama hiki kwenye klabu yangu."



# Griezmann aonya kikosi cha Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

ANTOINE Griezmann amesema Ufaransa inatakiwa kujifunza kutokana na kipigo cha kushtukiza cha mabao 2-0 kutoka kwa Finland wakati wakielekea kwenye mchezo dhidi ya Ureno, Jumamosi.

Mabingwa hao wa Kombe la Dunia kutofungwa kwao mechi 12 mfululizo kulifikia mwisho katika mchezo wa kirafiki uliochezwa juzi Jumatano pale kwenye dimba la Stade de France wakati walipofungwa mabao na Marcus Forss na Onni Valakari wenye umri wa miaka 21, ambapo hiyo ilikuwa mechi yao ya kwanza ya kimataifa.

Ushindi wa Finland ulikuwa ni wa kwanza dhidi ya Les Bleus hao, na mshtuko kwa kikosi hicho cha kocha, Didier Deschamps.

Marcus Thuram, alicheza kwa mara ya kwanza dakika zote 90 katika mechi ya kimataifa, ambapo mpira wa kichwa alioupiga uligonga mwamba na alishindwa kulenga goli wakati Finland wakiwa wanaongoza.

Deschamps alifanya mabadiliko nane kwenye kikosi chake kilichoanza katika mchezo wa ushindi dhidi ya Croatia mwezi uliopita, huku Griezmann akiwa mmoja wao walioingia wakitokea benchi na sasa wanakabiliwa na mchezo dhidi ya Ureno kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA, Jumamosi.

# Ramos aifikia rekodi ya Buffon Ulaya

**AMSTERDAM,** Uholanzi

LUIS Enrique amemsifia Sergio Ramos baada ya nahodha huyo wa Hispania kuifikia rekodi ya Gianluigi Buffon wa Italia kwa kuichezea mechi nyingi zaidi timu yake ya Taifa kwa bara la Ulaya, wakati wakitoka sare ya 1-1 na Uholanzi, Jumatano.

Ramos aliingizwa zikiwa zimesalia dakika tano kabla ya mpira kumalizika pale kwenye dimba la Johan Cruijff Arena na akacheza mechi yake ya 176 ya kimataifa, ikiwa ni miaka 15 tangu alipoanza kuichezea Hispania kwa mara ya kwanza.

Mlinzi huyo wa kati wa Real Madrid ameifikia rekodi ya Buffon kwa kuwa mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi za kimataifa kwa bara la Ulaya na ana nafasi ya kumpiku kama atacheza dhidi ya Uswisi pale Basel, Jumamosi.

Pia anashika nafasi ya nane duniani katika orodha ya wachezaji walioichezea Timu ya Taifa mechi nyingi zaidi, ambapo kwa sasa rekodi hiyo inashikiliwa na kiungo wa zamani wa Misri, Ahmed Hassan.

Kocha Mkuu wa Hispania, Enrique alimsifia Ramos kwa kuifikia rekodi ya Buffon.

"Sergio ni wa aina yake. Yupo katika levo tofauti kabisa," alisema kocha huyo baada ya mchezo huo.

"Rekodi ya kucheza mechi nyingi za kimataifa hufikiwa tu na wale waliobarikiwa sana."

Enrique katika mchezo huo aliwaanzisha wachezaji wengi wasio na uzoefu akiwamo golikipa, Unai Simon, pamoja na Koke, Alvaro Morata, Hector Bellerin na Marco Asensio.

Morata alimtengenezea pande Sergio Canales kuipa Hispania bao la uongozi dakika ya 18, likiwa ni bao la tisa kwa straika huyo wa Juventus kuhusika katika klabu na nchi yake msimu huu.



## HABARI MICHEZO

# Verratti aanza mazoezi na PSG

**PARIS,** Ufaransa

MARCO Verratti amepona majeruhi yake ya nyama za paja na amerudi kwenye mazoezi katika kikosi cha Paris Saint-Germain, Jumatano.

Kiungo huyo alirudi kutoka kwenye mechi za kimataifa Oktoba na maumivu hayo na amekosa mechi saba katika mashindano yote.

Kurudi kwake kutaongeza nguvu kwa kocha wa PSG, Thomas Tuchel, ambaye amekuwa akikabiliwa na wachezaji wengi muhimu ambao ni majeruhi msimu huu.

Verratti alianza mazoezi mepesi binafsi na Mauro Icardi anatarajiwa kurudi wiki hii.

PSG imeshinda mechi zote tano za Ligue 1 bila Verratti msimu huu, huku kiungo huyo wa Italia alikuwapo katika mechi mbili za mwanzo za kichapo mwanzoni mwa msimu huu.

Kati ya wachezaji wote waliocheza angalau mechi 10 za Ligue 1 msimu uliopita, ni Leandro Paredes pekee ndiye aliyeweza kuwa na pasi zilizokamilika nyingi zaidi kuliko Verratti ndani ya dakika 90.





# JESUS: BRAZIL ISIMTEGEMEE NEYMAR TU

**SAO PAULO,** Brazil

GABRIEL Jesus anataka Brazil kuthibitisha tena wanaweza kushinda bila Neymar baada ya kuthibitishwa kwamba nyota huyo ataukosa mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Venezuela.

Namba 10 huyo wa Brazil anasumbuliwa na maumivu ya nyonga, akikosa mechi tatu zilizopita za Paris Saint-Germain kwenye mashindano yote, ukiwamo mchezo wa kichapo kwenye Ligi ya Mabingwa dhidi ya RB Leipzig.

Brazil imekuwa kama inamtegemea zaidi nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ambaye alikosa mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ujerumani kwenye fainali za mwaka 2014, waliponyanyaswa kwa kuchapwa mabao 7-0.

Lakini kikosi hicho cha kocha Tite pia kilikuwa bila Neymar kwenye mashindano ya Copa America ya mwaka jana, ambapo walishinda taji, na Jesus aamini kama kikosi chake kinaweza kutafuta sababu.

"Ni kawaida kuzungumzia kuhusu umuhimu wa Neymar kwa klabu yake na timu yetu ya taifa, namna gani amejitoa na anachokitoa kila siku," alisema fowadi huyo wa Manchester City. "Mimi ni shabiki wake mkubwa.

"Lakini linapokuja suala la timu ya taifa, kila mmoja anatakiwa kubeba jukumu lake, sio kuachiwa yeye tu. Kila mmoja yupo hapa kwa sababu.

"Tukiwa na Neymar, huwa tunakaribia ushindi, lakini Brazil inatakiwa kuonyesha kwamba tunaweza kushinda bila yeye."

# Pulisic arudi kambini Chelsea

**LONDON,** England

CHRISTIAN Pulisic amerudi Chelsea baada ya kuondolewa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Marekani kinachojiandaa na mechi za kirafiki dhidi ya Wales na Panama.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 aliitwa na timu yake hiyo ya taifa licha ya kutokichezea kikosi chake cha Chelsea tangu Oktoba 28 kwa sababu ya kusumbuliwa na maumivu ya nyama za paja aliyoyapata kuelekea mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Burnley.

Hata hivyo, Pulisic hakuwa fiti kucheza dhidi ya Wales, mchezo uliopigwa pale Swansea, jana Alhamisi na hataweza kuwa pia kwenye mchezo dhidi ya Panama utakaopigwa nchini Austria, Jumatatu, na sasa ameondolewa kikosini.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana, Kocha Mkuu wa Marekani, Gregg Berhalter, alisema: "Christian ni sehemu kubwa ya kundi letu.

"Amekuwa anapitia kwenye majeruhi, lakini alisema wazi kwamba anataka kuja kwenye kambi yetu, kuwa karibu na wachezaji wenzake na kuendelea kuwa kiongozi wa timu."

Pulisic amecheza mechi tano kwa Chelsea katika mashindano yote msimu huu kabla ya kuumia na alifunga bao katika mechi ya hivi karibuni wakati wakishinda magoli 4-0 dhidi ya Krasnodar kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alipoulizwa kama Pulisic atakuwapo kwenye mchezo wa Chelsea dhidi ya Newcastle United utakaopigwa Novemba 21, Berhalter alisema: "Ni ngumu kutabiri."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BABA AKANUSHA MESSI KUTUA PSG

●●● Mzazi wa mshambuliaji huyo aziita habari kuhusu usajili huo si za kweli ni ...

**BARCELONA,** Hispania

BABA mzazi wa mshambuliaji, Lionel Messi, Jorge, ameziita ni upuuzi ripoti kwamba amewasiliana na Paris Saint-Germain kuhusu nyota huyo wa Barcelona.

Messi mwenye umri wa miaka 33, ameendelea kuhusishwa na uhamisho wa kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga, huku mkataba wake ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu na tayari aliomba kuondoka kipindi cha majira ya joto kilichopita.

PSG, Manchester City na Inter awali zilikuwa zikihusishwa na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

**Lakini baada ya ripoti kudai Jorge amewasiliana na PSG kuhusu kuanza mazungumzo ya usajili wa Januari, baba yake mzazi amekanusha madai hayo.**

"Acheni kuandika habari za kipuuzi!" Aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram.

Messi ametumia muda wake wote wa kucheza soka la kulipwa katika klabu ya Barcelona, ambako ameshinda mataji 10 ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alitaka kuondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto kilichopita, kabla ya kuamua kubakia.

Messi amefunga mabao sita katika mechi 10 msimu huuu, yakiwamo matatu kwenye Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga.

Ingawa bado ni mwanzo tu wa LaLiga msimu huu, Messi hadi sasa hana pasi ya mwisho hata moja, huku nafasi mbili za kufunga alizozitengeneza katika kipindi cha dakika 90 ni chache zaidi tangu msimu wa 2012-13.

Kikosi cha Barcelona kinachonolewa na Ronald Koeman kipo nafasi ya nane kwenye msimamo wa LaLiga, kikipitwa pointi tisa na vinara, Real Sociedad lakini kina mechi mbili mkononi.

## ZISIKUPITE

### SON, SPURS WATETA

MABOSI wa Tottenham Hotspur wameanza mazungumzo na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Son Heung-min. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 anatarajiwa kupewa mkataba utakaomalizika ifikapo mwaka 2026 na utamfanya apokee mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Guardian)***

### GOMEZ MAMBO MABAYA

BEKI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Joe Gomez (23), anahofia anaweza kukosa mechi zote za msimu huu zilizobakia baada ya kupata majeruhi akiwa kwenye mazoezi ya kuitumikia nchi yake. ***(Mirror)***

### UNITED KUMUUZA DROGBA

MANCHESTER United inajipanga kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba ambaye ana umri wa miaka 27 ifikapo dirisha la majira ya joto mwakani. ***(Talksport)***

### RONALDO, NEYMAR KUPISHANA

JUVENTUS imefungua milango ya kubadilishana wachezaji ambapo iko tayari kumuuza winga wake Mreno Cristiano Ronaldo (35), kwa Paris St-Germain na kusababisha mshambuliaji wa Brazil, Neymar kutua klabuni kwake. ***(Tuttomercato - in Italian)***

### RONALDO ATAJWA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo, anatajwa huenda akarejea katika klabu yake ya zamani ya Manchester United. ***(ESPN Argentina, via Metro)***

### WIJNALDUM ANUKIA BARCA

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amemtaja Georginio Wijnaldum anaweza kuwa "mbadala hapo baadaye" katika kikosi hicho cha vigogo wa Hispania. ***(Sport)***

### AHMEDHODZIC SOKONI

CHELSEA iko katika mazungumzo na beki wa Malmo na Timu ya Taifa ya Bosnia, Anel Ahmedhodzic, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Evening Standard)***

### WIJNALDUM KIMEELEWEKA

KIUNGO wa Liverpool, Georginio Wijnaldum (30), yuko tayari kusaini mkataba mpya. Mkataba wa sasa wa nyota huyo raia wa Uholanzi na klabu hiyo ya Ligi Kuu England unatarajiwa kumalizika mwisho wa msimu. ***(Liverpool Echo)***

### MUNICH YAMBANIA ALABA

LIVERPOOL inatajwa kumwania beki wa Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba, lakini Bayern Munich imesema haitamuuza mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 28 ifikapo Januari, licha ya mkataba wake kumalizika ifikapo majira ya joto mwakani. ***(Bild - in German)***

### KONATE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imeonyesha nia ya kumsajili beki wa RB Leipzig Mfaransa, Ibrahima Konate (21) na kiungo raia wa Ufaransa, Christopher Nkunku, 22. ***(Bild - in German)***

### POCHETTINO SOKONI

ATHLETIC Bilbao imeonyesha nia ya kutaka huduma ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa Tottenham, Mauricio Pochettino kuongoza timu yao. ***(Marca - in Spanish)***

## Julio ahitaji mechi zaidi U-20

**Na Saada Akida**

BAADA ya kucheza mechi nne za kirafiki, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema kikosi chake kimeanza kupata muunganiko mzuri tayari kuelekea kwenye mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFAU-20) yatakayofanyika kuanzia Novemba 20 hadi Desemba 6, mwaka huu jijini Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jijini baada ya mechi ya kirafiki dhidi ya Sudan, Julio alisema anahitaji mechi nyingine za kirafiki kwa ajili ya kujimarisha na kupata kikosi cha kwanza kabla ya kuanza kwa michuano hiyo.

Julio alisema ili kuendelea kujijenga, kikosi chake kinatarajia kuvaana na African Lyon ya Ligi Daraja la Kwanza na kesho kitaikaribisha Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu Bara kwenye mechi nyingine za kirafiki.

"Bado timu yangu haikuwa na muunganiko mzuri, sababu kubwa ya wachezaji wangu kutoka nje kuchelewa kujiunga kambini, hivyo hata mechi yetu ya leo (juzi) dhidi ya Sudan umeona mabadiliko makubwa katika kikosi.

"Nimewapa nafasi wachezaji ambao hawakucheza mechi yetu ya kwanza ya kirafiki dhidi ya timu hiyo (Sudan), sababu kubwa ni kutafuta kikosi cha kwanza kitakacholeta ushindani katika michuano inayotukabili," alisema Julio.

Ngorongoro Heroes ilipata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya kwanza dhidi ya wageni hao na waliporudiana juzi walikubali kichapo cha idadi kama hiyo.

## KMC yajiimarisha kuwakabili Azam

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha KMC kimeanza rasmi mazoezi kujiandaa na mechi ya raundi ya 11 ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC itakayochezwa Novemba 21, mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa KMC, Habib Kondo, alisema kikosi chake kimeanza mazoezi mapema ili kujiimarisha kuelekea mchezo huo dhidi ya vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, utakaochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

"Tumeanza mazoezi siku ya Jumanne. Hii ni maalum kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya Azam ambayo naamini itakuwa ngumu. Tumefanya hivyo kwa ajili ya kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwenye mechi zilizopita iliyafanyika kazi yapungue au yaishe kabisa," alisema Kondo, mchezaji wa zamani wa Sigara.

Kocha huyo alisema pia uamuzi wa kutomtumia straika wake, Reliants Lusajo kwa dakika zote 90, unatokana na mchezaji huyo kuwa majeruhi kwa muda mrefu, hivyo anarejea taratibu.

KMC iko katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kujikusanyia pointi 15, ikiwa imeshinda mechi nne, sare tatu na kufungwa michezo mitatu.

# KAZE AFUNGUKA MBIO ZA UBINGWA

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema ni mapema sana kwa sasa kuanza kujiona wapo kwenye nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema pamoja na mwendelezo mzuri wa timu yake katika ligi hiyo wakiwa hajawapoteza mchezo hata mmoja, bado anaona kuna safari ngumu kuelekea kutwaa ubingwa.**



"Ni kweli lengo letu ni kuona tunatwaa ubingwa msimu huu, lakini niseme ukweli ligi bado, ni mapema sana kwa sasa kuanza kujiweka kifua mbele tutatwaa ubingwa, sio kwa Yanga tu hata kwa timu nyingine, muda bado sana," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema wataanza kuona uwelekeo wao wa kutwaa ubingwa kuanzia katika mzunguko wa pili wa ligi.

"Kama tutamaliza hivi mzunguko wa kwanza, na tukaanza mzunguko wa pili kama tulivyoanza mzunguko wa kwanza, baada ya michezo kadhaa tunaweza tukaongelea mwenendo wetu kuelekea kwenye ubingwa, kwa sasa nataka wachezaji wangu waweke umakini katika kila mchezo tunaocheza," aliongeza Kaze.

Mabingwa hao 'wa kihistoria' kesho wanatarajiwa kuanza tena mazoezi kujiandaa na mechi za ligi zitakazofuata baada ya mapumziko mafupi aliyoyatoa kocha wao.

Nyota wanaotarajiwa kuanza mazoezi hayo ni wale ambao hawapo kwenye majukumu ya timu za taifa, huku kikosi cha Yanga kikiwa na wachezaji sita kwenye Kikosi cha Timu ya Taifa 'Taifa Stars'.

Mpaka sasa Yanga imecheza michezo 10 na kushinda michezo nane, huku ikitoka sare mara mbili ukiwamo mchezo dhidi ya watani zao Simba, uliochezwa wiki iliyopita.

Katika msimamo wa ligi, Yanga yenye pointi 24 iko kwenye nafasi ya pili nyuma ya vinara Azam FC wenye pointi 25 wakati mabingwa watetezi, Simba wako katika nafasi ya tatu.




Nahodha wa klabu ya gofu ya Lugalo, Kepteni Japhet Masai (kushoto), akielezea maandalizi ya mashindano ya Waitara ya mwaka huu, ambayo yatafanyika hapa jijini, Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya Bia ya Serengeti, Mark Mugisha ambao ni wadhamini wao na Mwenyekiti wa klabu hiyo, Brigedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *SBL yadhamini gofu ya Waitara*

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wachezaji wa gofu 150 kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, wanatarajia kuchuana kwenye mashindano ya Waitara ambayo mwaka huu yanadhaminiwa na kinywaji cha Johnnie Walker (JW) kinachosambazwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL).

Akitangaza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Masoko wa SBL, Mark Mugisha, alisema udhamini wa JW kwenye mashindano hayo unalenga kukuza na kuendeleza mchezo wa gofu.

"SBL kupitia kinywaji cha kimataifa cha Johnnie Walker inayofuraha kuwa mdhamini wa mashindano ya gofu ya Waitara kwa mwaka huu. Udhamini huu unaonyesha nia yetu ya kusaidia maendeleo ya michezo hapa nchini," alisema Mugisha.

Mkurugenzi huyo aliongeza mashindano hayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2006, na hivyo ni michuano inayofanyika kwa muda mrefu zaidi hapa Tanzania na kuongeza kuwa JW inayofuraha kuwa sehemu ya mashindano hayo makongwe.

"Wakati tukisherehekea miaka 200 tangu kuanza kutengenezwa kwa JW ambayo kwa sasa ni wisky namba moja ulimwenguni, tunayofuraha kusafiri katika miaka yote hii tukiendelea kuwa imara na katika ubora ule ule," Mugisha alisema.

Naye Mwenyekiti wa klabu ya gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo aliishukuru SBL kwa kukubali kudhamini mashindano hayo na kuzitaka kampuni nyingine kujitokeza kusaidia mchezo wa gofu.

"Tunaishukuru sana SBL kwa mwendelezo wao wa kufadhili mashindano haya na mchezo wa gofu kwa ujumla. Kwa sasa tunaweza kusema SBL ndiyo mdhamini mkubwa wa mashindano haya," alisema Luwongo.

# Michezo

Ijumaa Novemba 13, 2020

Nipashe




Baba akanusha Messi kutua PSG UKURASA 22



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Kundi J dhidi ya wenzao wa Tunisia kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2021). **PICHA: TFF**

# STARS KIBARUANI UGENINI TUNISIA

## ●●● Ndayiragije atamba ameandaa 'suprise' kubwa kwa Waarabu hao licha ya...

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kutupa karata muhimu dhidi ya wenyeji Tunisia katika mechi ya Kundi J ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika itakayochezwa kuanzia saa 4:00 usiku jijini, Tunis.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, alisema kikosi chake kiko tayari na kamili kwa mchezo huo na wamejipanga kupata matokeo mazuri.**

Ndayiragije alisema wachezaji wote walioko Tunis wako katika hali nzuri na ameandaa kucheza soka la ushindani na kusahau historia ya wapinzani wao kwenye mashindano hayo.

Kocha huyo alisema wamekwenda huko kutafuta pointi tatu hivyo, watacheza soka la kushambulia, lakini wakijilisha ili kujiweka katika nafasi salama kwenye kundi hilo.

Alisema anafahamu mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu kila upande umejiandaa kupata matokeo mazuri na hasa unapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.

"Tumefanya maandalizi mazuri, ingawa Istanbul kulikuwa na baridi kali, tumefanya mazoezi muhimu kulingana na mechi iliyoko mbele yetu, kila mchezaji yuko tayari kuipigania timu, malengo yetu ya kwanza ni kutafuta ushindi, inawezekana," alisema kocha huyo wa zamani wa Mbao, KMC na Azam FC za Tanzania.

Mshambuliaji wa timu hiyo, Simon Msuva, aliliambia gazeti hili wachezaji wanaahidi kupambana ili kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

Msuva alisema katika michuano hiyo hakuna timu ndogo wala kubwa ndio maana kila upande hufanya maandalizi ili kupata matokeo chanya.

"Watanzania wazidi kutuombea, watuunge mkono, mchezo ni mgumu, lakini naamini kwa Mungu hakuna gumu linaloshindikana, kwa upande wetu tumejiandaa vizuri na tupo tayari kupambana," alisema Msuva.

Aliongeza wataingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao na si kuwahofia kwa sababu katika mpira lolote linaweza kutokea.

"Tumeshacheza mechi nyingi ngumu na zenye ushindani mbalimbali, hakuna mechi rahisi, tutaingia uwanjani kupambana kwa sababu tuna malengo ya kucheza tena Afcon mwakani, hakuna kisichowezekana kwenye soka, tunahitaji kulitangaza vyema jina la nchi yetu," Msuva aliongeza.

Katika mechi hiyo, Taifa Stars itashuka dimbani bila nahodha wake, Mbwana Samatta, ambaye alipata majeraha ya nyama za paja akiwa kwenye klabu yake ya Fernabahce ya Uturuki, mshambuliaji huyo pia atakosa mchezo wa marudiano utakaochezwa Novemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Tunisia yenye pointi sita ndio vinara wa kundi hilo wakifuatiwa na Equatoria Guinea yenye pointi tatu sawa na Libya na Taifa Stars inaburuza mkia, pia ikiwa na pointi tatu.

Taifa Stars ilianza kampeni ya michuano hiyo kwa ushindi dhidi ya Equatorial Guinea halafu mchezo wake wa pili ilikubali kichapo cha ugenini dhidi ya Libya.

# Mwakinyo, Paz kumaliza ubishi leo

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Hassan Mwakinyo anatarajia kupambana na Jose Carlos Paz kutoka Argentina katika pambano la ubingwa wa Mabara wa WBF wa uzito wa Super Welter litakalofanyika leo kwenye ukumbi wa Next Door Arena jijini, Dar es Salaam.

Mwakinyo ndio bingwa mtetezi wa pambano hilo la raundi 12 ambalo limeandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sport chini ya ukurugenzi na mwanzilishi, Kelvin Twissa na kusimamiwa na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC) na WBF.

Akizungumza jijini jana, Mwakinyo alisema anatarajia kuibuka na ushindi katika pambano hilo tena katika raundi za mwanzoni.

Bondia huyo kutoka jijini Tanga amewataka mashabiki wake kufika mapema kushuhudia akimchapa mpinzani wake huyo na kuendelea kuushikilia mkanda huo wa dunia akiwa kwenye ardhi ya nyumbani.

"Nataka kufanya staili ya mabondia wa zamani kama Mike Tyson ambaye alikuwa anamaliza pambano, huku mashabiki wengine wakiwa katika foleni ya kuingia na wengine wakikata tiketi. Nataka kuweka historia nyingine," alisema Mwakinyo.

Alisema ataingia ulingoni kwa kumpa heshima Paz, lakini amejiandaa kuhakikisha mpinzani wake huyo anaachana na mchezo wa ngumi za kulipwa kutokana na kipigo atakachompatia.

Paz alisema hana maneno mengi na badala yake Watanzania wasubiri kuona mikono yake ikiongea na kuthibitisha ubora aliokuwa nao.

"Mikono ndio itaongea ulingoni katika kuthibitisha ubora wangu, najua Mwakinyo anaongea sana, ni kawaida, lakini mimi nitaonyesha vitendo na kuondoka na mkanda huu," alisema Paz.

Mbali ya pambano hilo, bondia Hussein Itaba atachuana na Alex Kabangu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakati Mkenya Fatuma Zarika na Patience Mastara wa Zimbabwe watachuana kuwania mkanda wa dunia wa WBF uzito wa Super Bantam huku Mtanzania Zulfa Macho atazichapa na Alice Mbewe wa Zambia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >